# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Februari 4, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581576

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 14

**MANJANO, KIAZI INAVYONG'ARISHA NGOZI**

**Makonda** aonya mgogoro viongozi, atishia kuvunja baraza madiwani

UKURASA 2

**Mzee** Mwinyi alazwa, watu wamwombea



UKURASA 5

**Wafariki** dunia kwa kupigwa radi wakitazama mpira

UKURASA 5

# Mambo 8 yaliyotikisa Bunge ndani ya siku 4

UKURASA 4



PATROBAS KATAMBI



SPIKA WA BUNGE TULIA AKSON



DK. JOSEPH MHAGAMA



NEEMA LUGANGIRA



STELLA MANYANYA

# Rais Samia asisitiza mawaziri kuzingatia maslahi ya taifa

• **Ni** katika miradi mikubwa inayotekelezwa nchini

*Endelea Ukurasa 2*



# Mvua yazidi kuleta maafa

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YAIZIMA MASHUJAA BARA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Samia asisitiza mawaziri maslahi ya taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza mawaziri kuzingatia maslahi ya taifa na ya wananchi kwenye miradi mikubwa inayotekelezwa nchini.

Pia ameagiza serikali kujiimarisha kwenye kampuni kwa kuongeza umiliki wa hisa kama ilivyofanyika kitalu cha Mnazibay. Kwa sasa kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), serikali ina hisa asilimia 40 huku kampuni ya Maurel & Prom ikimiliki asilimia 60.

Akizungumza jana kwenye hafla ya utiaji saini mauziano ya hisa za kampuni ya Wentworth Resources PLC katika kitalu cha Mnazibay baina ya TPDC na kampuni ya Maurel & Prom, Rais Samia alisema ni muhimu kutanguliza maslahi ya taifa badala ya maslahi binafsi katika miradi hiyo.

"Kama mwanadamu unajua unaweza kuona hapa kuna ngoja nitumbukize. Maslahi ya taifa yawe mbele na si ya mtu mmoja mmoja,"alisema.

Rais alisema suala la wenyeji kujishughulisha kiuchumi katika kutekeleza yatokanayo na miradi mbalimbali (local content) na mradi kurudisha hisani kwa wananchi (CSR) limekuwa likilalamikiwa utekelezaji na kuagiza lisimamiwe kikamilifu.

"Sera ya 'Local Content' baadhi ya kampuni kubwa zinatengeneza mazingira ya wananchi kutoingia kwenye mnyororo wa usambazaji au wa utoaji wa huduma kwenye kampuni hizo.

Hii si haki, ni lazima tubainishe maeneo ambayo sera hii inatakiwa kutumika na itumike kikamilifu.

"Tumesikia msemaji wa kampuni hii tayari amefanyia kazi eneo hili na kwa upande wa kurudisha hisani kwa jamii hapa napo kumekuwa na mambo mawili.

Kwanza, kampuni zinatoa zinavyojisikia kutoa, hatujasimama bado na kusema kampuni ya mtaji gani itoe kiasi gani kwa wananchi. Hili liende kufanywa kazi na hata hicho wanachojisikia kutoa hakisimamiwi ipasavyo"alisema.

Aliwaagiza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, na wenye dhamana katika miundombinu na sekta zote zenye miradi mikubwa kusimamia suala hilo.

"Yale yote yanayosababishwa na udhaifu wetu kwenye masuala ya CSR na 'local content', twende tukarekebishe ni kwa wote si sekta hii peke yake. Nafahamu kuna miradi inatoa kwa wananchi lakini zikiingia fedha halmashauri, hisani haifiki kwa wananchi. Yanafanyika mengine hapo katikati.

"Niliona kwenye habari kuna wananchi wa kijiji kimoja kule mara kuna mgodi mkubwa wa dhahabu wanalia na kituo cha afya.

Mradi upo pale miaka kadhaa huwezi kumlaumu mwekezaji, unalaumu halmashauri ambao wamepokea fedha na kutumia kinyume cha matakwa ya wananchi," alisema.

"Lazima wananchi wanufaike na matunda ya uwekezaji kwenye maeneo yao. Kwa sekta ya gesi lazima wananchi wa Lindi na Mtwara waanze kuona manufaa ya uwapo wa kampuni kubwa kupitia CSR na ajira," alisisitiza.

Alisema anaamini ajira zisizo za kitaalamu sana zitakwenda kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo na kuwepo na mipango ya wananchi kutoa huduma ili kukua kiuchumi.

"Suala la kuwa na gesi majumbani si anasa. Ni suala ambalo serikali tunawajibika kutoa huduma hiyo kwa wananchi kupitia sekta binafsi kwa mipango tutakayoweka vizuri. Nimefurahi kusikia katika mipango yao ni kusogeza gesi kwa wananchi," alisema.

Alisisitiza kuwavuta wawekezaji kuwekeza kwenye gesi kwa kuhakikisha serikali inakuwa na umiliki wa maamuzi kwenye rasilimali.

Awali, Rais Samia alibainisha shughuli za utafutaji wa gesi asilia kuanza nchini na visima 96 vimechimbwa na kati ya hivyo, 59 viko nchi kavu na 37 baharini huku 43 vikiwa viligundulika kuwa na gesi inayokadiriwa kufikia futi za ujazo trilioni 57.54.

"Maeneo ambayo uzalishaji wa gesi unaendelea ni Songosongo na Mnazi Bay ambapo kwa siku tuna uwezo wa kuzalisha futi za ujazo milioni 245 wakati mahitaji halisi kwa sasa ni milioni 297. Hii inachangia kuongeza uzalishaji wa umeme nchini ambao kwa wastani unaozalishwa kwa kutumia gesi asilia ni takribani asilimia 65 hadi 70 ya umeme wote nchini," alisema.

Alisema tayari viwanda 56 vimeunganishwa na vinatumia gesi asilia nchini wakati vingine vimeomba na vinasubiri kuunganishwa.

Rais alisema gharama za uchimbaji visima ni kubwa na huongezeka zaidi wakati wa uchorongaji wa visima na kwamba kwa kisima kimoja, inafikia Dola za Marekani milioni 40 na gharama uendelezaji kitalu cha Mnazi Bay kaskazini ni Dola milioni 55, sawa na bajeti za wizara mbili kwa mwaka mzima.

Kuhusu mauziano ya hisa, Rais Samia alisema: "Nilimweleza Waziri lazima tununue asilimia 20 ya hizo hisa iwe iwavyo kwa sababu tuna mbia ambaye yuko madhubuti. Nilijua fedha hizi tunazoziingiza hazitapotea na baadaye zitakuwa na manufaa makubwa.

Sasa tuna umiliki wa asilimia 40 ambao unatupa nguvu ya kusema yetu kwenye hili. Sisi serikali hili si jambo dogo ni jambo kubwa na ni la kwanza kwa sababu tumekuwa tukipitishiwa makaratasi kampuni za nje kuuziana zenyewe kwa zenyewe," alisema.

Ili kufanikisha hilo, alisema watendaji 100 wa TPDC watajengewa uwezo ili kushiriki katika shughuli za gesi asilia kwa vitendo.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisisitiza serikali kuendelea kuongeza umiliki wa hisa kwenye rasilimali za taifa huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alimhakikishia Rais kuwa mradi huo utatekelezwa kama ilivyopangwa na kusisitiza kuwa hawatamwangusha.

Dk. Biteko alisema kupitia CSR wananchi wa Madimba watajengewa kituo cha afya, polisi, barabara, taa za barabarani na gari la kubebea wagonjwa na kwa Songosongo umeme, maji vitapelekwa.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Mussa Makame, alisema mikataba hiyo ni mkataba wa mauziano ya hisa za iliyokuwa kampuni ya Wentworth ambayo imeuza na kununuliwa na kampuni ya Maurel & Porm na TPDC.

Alisema mkataba mwingine ni wa uendeshaji wa kitalu cha Mnazi Bay ambapo ugawanyaji wake wa mapato kati ya serikali ya Tanzania, TPDC na Wentworth ulitiwa saini Mei, 2004 na hadi sasa kuna hifadhi ya gesi inayoweza kuzalishwa kiasi cha futi za ujazo bilioni 641.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
04.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **06-02-2024 hadi 08-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar- Es- Salaam Port** kuelekea **Mzenga**, gari hizo zina namba za usajili:

**T 116 EDS / T 879 EAU**
**T 118 EAG / T 881 EAU**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22.00**
**Upana - mita 7.50**
**Kimo - mita 4.60**

2. Njia itakayotumika: Bandari ya Dar-Es-Salaam hadi Mzenga kupitia Morogoro Road

Gari zitasafiri muda wa usiku **(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)** Kutoka **Dar- Es- Salaam Port** mpaka **Mlandizi**

Kutoka Mlandizi kwenda **Mzenga** gari zitasafiri muda wa mchana **( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# Makonda atishia kuvunja baraza madiwani

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** KIGOMA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amewaonya viongozi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji kwamba endapo hawatabadilika, atapendekeza kuvunjwa kwa baraza la madiwani.

Makonda aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kigoma katika mwendelezo wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na kutatua kero za wananchi.

Aliwapa onyo la mwisho viongozi wa Manispaa ya Kigoma kuhakikisha wanafanya kazi kwa kushirikiana badala ya kuendeleza malumbano yanayosababisha wananchi kukosa maendeleo.

"Kumekuwa na malumbano ya madiwani na watendaji, kila mtu kuwa na mtu wake wa kumpa tenda inakwamisha maendeleo ya wananchi wa Kigoma, wana mivutano isiyokuwa na tija inayoongozwa na ubinafsi na zaidi ya yote ni upigaji," alisema

Alisema mvutano huo unasababisha kukosekana kwa maendeleo na endapo wakiendelea kupata taarifa watakaa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (TAMISEMI) na kupeleka mapendekezo kwa Mwenyekiti wa chama ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan, kulivunja baraza la madiwani na kuweka uongozi wa mpito.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuwasaidia wananchi wa Kigoma kupata maendeleo na wanataka viongozi waliochaguliwa na walioteuliwa wawe na kauli moja ya kuwahudumia wananchi.

"Hili nimeona niliseme hadharani ili mstahiki meya na madiwani wenzake, watendaji mliopo pamoja na Mkurugenzi muende kutafuta namna ya kufanya kazi kama timu moja hawa wananchi wanataka maendeleo hawataki malumbano,"alisema Makonda.

Aidha, Makonda ameagiza ofisi ya Mkuu wa Mkoa kufunguliwa ofisi kesho (Jumapili) na watendaji wote wa Kigoma vijijini na mjini wafike kwa ajili ya kutatua kero za wananchi na yeye atapita kufuatilia.

"Ninahitaji kila mmoja asikilizwe ili tupate haki za wananchi tunachokitaka ni wananchi kutatuliwa kero zao na sio viongozi kuendelea kulumbana,"alisema Makonda.

Aidha, Makonda alisema walipokuwa Wilaya ya Kasulu, kuna diwani wa Kageramkanda, Ezekiel Kabonge, aliyesimamishwa kwa miaka mitatu na uchaguzi haujafanyika.

Awali Kabonge alidaiwa amefanyiwa vitimbi kwa madai kuwa si raia wa Tanzania na alikwenda kufungua kesi na kupatiwa ushindi kuwa Mtanzania kutokana na hukumu iliyotolewa na jaji.

Alisema licha ya kupatiwa hukumu ameendelea kuzuiwa kuwa diwani hali iliyosababisha wananchi wake wakose maendeleo katika kata hiyo kutokana na mgogoro unaoendelea na kuomba kurudishiwa uongozi wake.

Aidha, Makonda alisema amefanya mazungumzo na viongozi wa serikali wote kwa pamoja wamekiri kata hiyo inatakiwa kuwa na mwakilishi ni makosa kutokuwa na mwakilishi.

Alisema kwa kuwa mwakilishi yupo kwa mujibu wa katiba walichokubaliana na viongozi wa serikali wataleta timu kutoka taifa itakayokuwa chini ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

"Timu hiyo itachunguza mambo yote ya migogoro ya ardhi iliyopo kwenye mipaka, migogoro ya vitalu, mashamba na kwa sababu kuna timu ya mawaziri ilishapita ikaandika ripoti timu hiyo itajiweka mahusus kwa mkoa wa Kigoma ili kuhakikisha wananchi wanapata majibu kwa wakati,"alisema Makonda.

## HABARI KITAIFA

# Mafuriko yazidi kuleta maafa maeneo mbalimbali

**Na Waandishi Wetu**

MAFURIKO yanayotokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, yameendelea kusababisha maafa kwa kuharibu nyumba huku mazao na mali zikisombwa pamoja na baadhi ya huduma kufungwa.

Katika taarifa zilizotolewa kutoka baadhi ya maeneo nchini, zaidi ya nyumba 100, mashamba yenye mahindi na maharage vimesombwa na maji katika Kata ya Mbalagani, Maswa mkoani Simiyu.

Aidha, baadhi ya wananchi wamejeruhiwa baada ya kuporomokewa na kuta za nyumba zao.

Diwani wa Mbalagani, Abel Masunga, alisema juzi kuwa mvua hiyo iliyonyesha kuanzia majira ya asubuhi, ilisababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara pamoja na mazao yaliyofunikwa na maji kutoka katika mto uliofurika na kumwaga maji katika makazi ya watu.

"Mashamba ya wananchi, miundombinu na nyumba ni sehemu ya vitu ambavyo vimepata madhara katika kata yangu. Tunaomba serikali kututazama na kutusaidia kutuwezesha msaada ili kurejesha matumaini ya wakazi wa mtaa huu," alisema.

Wakieleza hali ilivyokuwa, baadhi ya waathirika wa mvua hizo walisema janga hilo lilitokea juzi majira ya saa 7:00 mchana baada ya mvua kukatika na maji ya mto kuacha njia na kufuata makazi ya watu.

Mkazi mwingine, Zingola Mafule, aliiomba serikali na wadau mbalimbali kuzisaidia kaya hizo hususani kwa watoto wanaotakiwa kuendelea na masomo ili wapate haki yao ya msingi.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyonge, alifika katika eneo hilo na kutoa tahadhari kwa wananchi hao hususani wale wenye nyumba ambazo si stahimilivu kuhama.

"Mto umefurika sana kwa kipindi hiki ambavyo haijawahi kutokea. Niwaombe mchukue tahadhari kwani leo hii mali zetu zimesombwa na nyumba kubomoka watu hawajadhurika zaidi kutokana na kuwa madhara yametokea mchana, hivyo tusisubiri hatari zaidi za kibinadamu,"alisema Kaminyonge.

Katika hatua nyingine, wakazi wa Kijiji cha Songambele Kata ya Ipalamasa wilayani Chato, mkoani Geita, wameingiwa na hofu baada ya kutokea mlipuko wa maji ulioambatana na moshi na tope lililofunika hekta 17 za mazao na baadhi ya nyumba.

Mmoja wa wakazi hao, Flora Benjamin, alisema hali hiyo ilianza kama mvuke ndipo yakaanza kutoka maji yaliyoanza kuteremsha miti na tope kuelekea katika maeneo ya mashamba ya mpunga na makazi.

Kutokana na hali hiyo, mmoja wa wakazi, Faustine Mbasa, aliomba serikali kupeleka wataalamu wa miamba katika eneo hilo na kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha mlipuko wa tope hilo ambalo limetokea ghafla katika mashamba yao.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Deusdedith Katwale, alifika katika eneo hilo na kuahidi kupeleka wataalam wa miamba ambao watasaidia kuhakikisha wanachunguza suala hilo na kubaini endapo kuna madhara yanaweza kujitokeza ili yadhibitiwe mapema au kuchukua tahadhari.

**SHULE YAFUNGWA**

SERIKALI ya Wilaya ya Morogoro imeifunga Shule ya Msingi Juhudi iliyopo Kata ya Lukobe Manispaa ya Morogoro ikiwa ni hatua ya kuchukua tahadhari dhidi ya madhara yanayoweza kutokea tena kutokana na mvua zinazonyesha maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Uamuzi wa kuifunga shule hiyo ni kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na walimu dhidi ya mafuriko ambayo yametokea mara kadhaa shuleni hapo.

Baada ya kufungwa kwa shule hiyo, Januari 30 mwaka huu Kamati ya Wataalamu ya Halmashauri ya Manispaa Morogoro (CMT) ikiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ally Machela, imeridhia kujenga shule mpya ya msingi ya dharura.

Shule hiyo mpya itajengwa katika eneo la Shule ya Sekondari Tushikamane iliyopo katika Kata ya Lukobe.

Machela alisema uamuzi wa Manispaa ni kuhakikisha wanafunzi wa Shule ya Msingi Juhudi wanaendelea na masomo baada ya shule hiyo kufungwa.

Alisema kwa kuanza zitatolewa Sh. milioni 25 kwa ajili ya kukamilisha maboma mawili yaliyopo katika Shule ya Sekondari Tushikamane kwa ajili ya kusoma wanafunzi wa darasa la awali 53 pamoja na ofisi ya walimu.

Januari 25 mwaka huu Shule ya Msingi Juhudi iliyopo Kata ya Lukobe ilikumbwa na mafuriko.

Kabla ya kufungwa kwa shule hiyo, Shirika la Kimatafa la Humanity First Tanzania (Utu kwanza) kwa kushirikiana na Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania lilitoa vijana kwa ajili ya kusafisha vyumba vya madarasa vilivyojaa tope ili kuwezesha wanafunzi kuendelea na masomo.

Hata hivyo, imeonekana eneo hilo si salama tena kuwapo kwa shule hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebeca Nsemwa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama alilazimika kuchukua hatua ya kuifunga shule hiyo ikiwa ni tahadhari dhidi ya madhara yanayoweza kutokea tena.

**- Imeandikwa na Vitus Audax (MASWA na CHATO) na Ashton Balaigwa (MOROGORO).**


## NOTISI YA MNADA WA HADHARA/MARUDIO YA TANGAZO

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED** kwa idhini na mamlaka tuliyo pewa na **MWANGA HAKIKA BANK,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara wa mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini, Mnada utafinyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi nne (14) au siku saba (7) kuanzia tarehe ya notisi / tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAULO J. MUHIRI | PAUL JULIAS WANGUBO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.ILA 029742 | KIPUNGUNI B, KITUNDA, ILALA MUNICIPALITY, DAR ES SALAM | TAREHE 13/02/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 2 | KAISER ALLOYCE KINYANGASI | KAISER ALOYCE KINYANGASI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO YA KIWANJA KUTOKA SERIKALI YA MTAA | MBWATE, KIBAHA,PWANI | TAREHE 24/02/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhu siwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali iliyopo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyo fikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne(14) toka tarehe yam nada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki(transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank(eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 1305**
**Songea,Ruvuma**
**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298/ 0784 718 734**
**Email:twinscoltd5@gmail. com**

# Mambo manane yaliyotikisa bunge siku nne

**Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE moto. Ndivyo ilivyokuwa kutokana na mjadala mkali ndani ya siku nne katika Mkutano wa 18 wa Bunge unaoendelea jijini Dodoma. Ni mjadala uliotikisa vichwa vya wanasiasa, wanaharakati na wadau mbalimbali huku mambo manane yakishuhudiwa kuibuka ikiwamo mvutano wa wabunge hasa katika suala la uundwaji wa Tume Huru ya Uchaguzi.

Mengine yaliyotawala mjadala huo ni Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC). Baada ya mjadala mrefu, ikakubalika kuwa vigogo hao wanaobeba hatima ya uchaguzi nchini, sasa hawatateuliwa moja kwa moja na Rais kama ilivyokuwa awali, kwa sheria iliyopitishwa na bunge, sasa watapendekezwa kwa Rais na Kamati ya Usaili.

Mambo hayo yaliibuka katika mjadala wa miswada ya sheria tatu zilizowasilishwa bungeni ambazo ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na Sheria ya Vyama vya Siasa, zote za mwaka 2023.

Jambo lingine lililotikisa mjadala wa Bunge ni katika muswada wa Sheria ya Uchaguzi kuhusu wakurugenzi wa halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji kusimamia uchaguzi. Baada ya mjadala mrefu, ilikubaliwa kwamba si lazima wawemo bali mtumishi yeyote mwandamizi wa umma anaweza kuwa msimamizi.

Kupitishwa kwa miswada hiyo, sasa hatua inayosubiriwa ni Rais Samia Suluhu Hassan kutia Saini wakati wowote na hatimaye kuwa sheria. Hatua hiyo pia imetoa mwanya au mawanda mapana zaidi ya namna gani makamishna wa NEC wanaweza kuteuliwa pamoja na wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo mbalimbali nchini.

Pia kuna suala la NEC kusimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na ule wa Serikali za Mitaa. Katika hilo, serikali imeridhia maoni ya wadau mbalimbali nchini, vikiwamo vyama vya upinzani, viongozi wa dini, asasi na mashirika ya kiraia, baada ya kushauriana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuunganisha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

**VITI MAALUM**

Wakati wa kupitia marekebisho ya serikali, katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, kulijitokeza mvutano mkali kuhusu uteuzi wa wabunge na madiwani wa viti maalumu.

Akiiongoza Kamati ya Bunge zima kupitia kifungu kwa kifungu, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema serikali imependekeza kifungu kipya cha 114, ambacho NEC, baada ya kushauriana na Msajili wa Vyama vya Siasa, inaweza kutoa mwongozo kwa vyama vya siasa kuhusiana na mwongozo wa kuchagua wagombea wanawake wa viti maalumu.



Dk. Joseph Mhagama



Dk. Tulia Ackson



Salome Makamba

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, akichangia jambo hilo, alisema mwongozo huo ni kuhusu upatikanaji wa wagombea wa viti maalum wa ubunge na udiwani, lakini mwongozo unaotakiwa ni wa namna ambavyo mchakato unatakiwa ufanyike ndani ya vyama kwa kuzingatia mambo ya jinsia.

"Tunataka kuweko na jinsia kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali tofauti na sasa hivi. CCM kwa mfano, ina wabunge wa vyuo vikuu, wanaotokana na NGO (mashirika yasiyo ya kiserikali). Huku kwetu CHADEMA, tunachagua wabunge wa mikoa na wabunge wa vijana.

"Ni lazima tuwe na mwongozo sawa ambao utakuwa na sura ya kitaifa wa namna ambayo wabunge wa viti maalumu wanapaswa kupatikana ili kuondoa upendeleo, rushwa, mazingira ya namna hiyo. Tunatamani Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume, watupatie standard form (mfumo unaofanana), ambao mimi nikisema naenda kugombea CHADEMA leo sina wasiwasi," alisema.

Kauli hiyo ilijibiwa na Spika Dk. Tulia ambaye alisema hakuna haja ya kutaka tume na msajili alisema kuviamulia mambo kwa kuwa huo ni utaratibu wa ndani ya chama katika kupata wawakilishi wake.

Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisimama na kusema suala si kwamba wataenda kuingilia vyama, wanafahamu kwamba Msajili wa Vyama ndiye baba anayesimama katikati kuhakikisha vyama vyote vinafanya sawasawa na katiba zao.

"Kwa hiyo sisi tunafikiria kwamba, kama wanawake tukiwa na uniform ya kupata viti maalumu vya wanawake, tutapunguza malalamiko na uonevu, ambao tunafikiri wanawake wajao wa miaka ijayo wasije kuyapata.

"Tunapozungumzia fomula moja tutengeneze; na labda niongezee jambo moja hapo isiwe Msajili wa Vyama, wawekwe na viongozi wa vyama pia, waambiwe kwamba utaratibu wetu wa kupata viti maalum ni huu hapa," alisisitiza.

Spika alilazimika kutoa ufafanuzi na kusema: "humu ndani vyama vikubwa vilivyomo, kuna uwakilishi wa Wabunge wa Viti Maalum ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama cha Mapinduzi (CCM). Chama cha Mapinduzi, wabunge wanawake wanaoenda kugombea majimboni, ukishindwa huji humu ndani (Bungeni).

"Wabunge wa CHADEMA, Viti Maalumu, ukienda kugombea jimbo na jina lako linakuwapo kwenye orodha. Ni taratibu ambazo kila chama kimejiwekea namna ya kuleta watu humu ndani. Sasa hayo mnataka yakaamuliwe wapi zaidi ya ndani ya vyama vyenu?"

Katika kutetea hoja hiyo, Neema Lugangira (CCM), alisema: "Nami nisisitize kwamba tuliridhia kuondoa yale mapendekezo ya kamati kwenye 112 na 113 (kifungu), kwa sababu serikali ilikuwa imeleta mapendekezo kwenye 114, ambayo Spika ulituambia kinaweza yakabeba yote mawili.

"Lakini nikirejea kwenye ibara ya 81 kinachoweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa, kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina ya aina ya Wabunge waliotajwa katika ibara ya 66 (1) b na ukirejea hapo utaona hapo inaongelewa wa Viti Maalum. Kwa hiyo hiki tunachojaribu kukiongelea hapa ni kwamba, basi tume itekeleze jukumu lake la kikatiba ambalo liko kwenye katiba."

Mvutano huo ukamwibua tena Spika akisisitiza yuko pale pale kwamba NEC yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu.

"Sasa hivi Tume ya Uchaguzi imeweka masharti au hayapo? Mmefikaje humu ndani Wabunge wa Viti Maalum kama tume haijaweka?" alihoji.

Alipomaliza kuhoji jambo hilo, Lugangira aliendelea kujenga hoja yake akisema: "Hapa hoja kubwa na msingi wa hoja ni utaratibu unaofanana. Yaani tunachojaribu kufanya ni kwamba kuwe na utaratibu unaofanana wa namna ya kuwapata hawa wawakilishi wa viti maalum."

Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Agness Hokororo, aliposimama aliungana na wachangiaji wengine, akisema haoni madhara katika hoja hiyo ya uteuzi wa wabunge na madiwani wa viti maalum.

"Mheshimiwa Mwenyekiti (Dk. Tulia), nataka kujibu swali lako, je vyama vinaingiliwa? Jibu ni hapana kwa kufuata muktadha wa ibara ya 81. Kifungu cha 114 kilichopendekezwa kinasema tume inaweza. Kwa hiyo sioni madhara. Umefafanua vizuri kwamba vyama hivi viwili ambavyo vina wabunge kwamba pengine kule wana huo utaratibu na huku kuna huo utaratibu.

"Tukumbuke wakati mwingine hawa wabunge wa viti maalum kwa utaratibu huu ambao sasa hivi vyama vinavitumia, utaratibu wa ndani ya chama changu (CCM) ni murua kabisa na madhubuti kabisa, tunaukubali kwa asilimia 100.

Akifafanua zaidi hoja kuhusu uteuzi huo, Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya, alisema kwa mara ya kwanza, wabunge wanawake wamejitahidi sana kwenda sambamba na miswada hiyo ili kujitahidi kuangalia changamoto zote zinazolikabili kundi la wanawake.

"Lengo la sheria zinazotungwa ni kurekebisha mapungufu ambayo yalikuwa yanaonekana katika maisha ambayo tulikuwa tayari tumeshayapitia, tumeshayaona. Kwa hiyo tukaona kwamba, kwa sababu tume inayo hiyo nafasi ya kufanya hivyo. Na hapa tunalozungumzia ni la mtu huyu mwanamke atakayekuwa kwenye kundi la viti maalum.

"Ni vyema hizi changamoto, huko kwenye chama tukisema tu tunawaachia ni sawa, lakini kuna suala la msingi la haki za binadamu, suala la msingi la haki za huyu mwanamke au jinsia kwa ujumla wake," alisema.

"Kwa hiyo, kwa msingi huo sisi tunaona kwamba, ukiwekwa utaratibu mzuri kwa vyama, ambao ukiacha leo kwa CCM ambao hatuna shida kubwa, lakini kwa CHADEMA, na kuna vyama vingi tu, tumesema viko 19 vyenye usajili wa kudumu. Ni vyema kuweka msingi ambao unaleta maridhiano, unaleta kujenga, kurekebisha na kujenga upya," alisisitiza.

Baadae, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Hadija Taya (Keysha), alisimama na kusema: Kama walivyosema wenzangu, katiba inaruhusu NEC, vyama vya siasa vipendekeze na kutoa utaratibu wa kuchagua kutekeleza jambo moja lakini jambo la kuchagua bado kwa sababu bado katiba inaruhusu nadhani ni vizuri sisi Wabunge tukatengeneza sheria nzuri.

"Kwa sababu hii inaenda kumsaidia mwanamke au Wabunge wa Viti Maalum kuonekana kama si Wabunge, wapo wapo tu. Wabunge ambao ni heshima na wamegombea kwa utaratibu mzuri ambao umetengenezwa na sheria ambayo tunakwenda kuitengeneza leo."

Mvutano huo ulimwibua Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, ambaye alisimama na kulieleza Bunge kuwa: "Hili jambo ndio maana upande wa serikali tulisema tunaondoa kwa sababu tunazo sababu... ukirudi kwenye sheria ya msingi, inaeleza kwamba kama ataleta nje ya utaratibu na akawa amekiuka haki za binadamu na hisia zote ambazo ni 'genuine' za wabunge, maana yake bado sheria nyingine zitatumika kuamua."

Dk. Joseph Mhagama, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, alisimama akisema: "Kamati ilishauriana na serikali, lakini nimeshangaa kuona serikali kwa nini wanataka kuondoa kifungu ambacho wamekileta.

"Madhumuni ya kamati ni kuwa na utaratibu wa wazi na si utaratibu unaofanana. Kwa hiyo CCM, natolea mfano, utaratibu wa kupata viti maalum ni huu, kwa hiyo tume na msajili wa vyama vya siasa wajue utaratibu wa Chama cha Mapinduzi ni huu.

Mwanachama wa CCM ambaye aligombea nafasi hiyo akaikosa, kwa sababu utaratibu haukufuatwa, awe na fursa ya kulalamika kwa chombo kinachosimamia hizo taratibu. Kadhalika kwa vyama vingine na haikulenga chama chochote, ililenga vyama vyote vya siasa viweke utaratibu wa wazi na sio unaofanana."

## HABARI KITAIFA



Mbunge wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akisisitiza jambo wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Sitalike- Kibaoni, Mlele mkoani Katavi jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Pinda alia kasi ndogo ujenzi barabara

**Na Munir Shemweta,** KATAVI

MBUNGE wa Kavuu, Geophrey Pinda, amemlilia Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, kutokana na uchelewеshaji ujenzi wa barabara kutoka Kibaoni- Sitalike yenye urefu wa kilomreta 70 katika Halmashauri ya Mpimbwe, Mlele mkoani hapa.

Barabara hiyo inayojengwa na Kampuni ya China Railway Seventh Gruop Co Ltd ujenzi wake uliianza mwishoni mwa mwaka 2022 na kutarajiwa kukamilika mwaka huu.

Pinda ambaye ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alitembelea eneo la barabara hiyo jana ikiwa ni sehemu ya ziara ya jimboni kwake iliyolenga kufanya ukaguzi wa shughuli za maendeleo pamoja na kuwajulia hali wananchi waliopatwa na ugonjwa wa kipindupindu.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, barabara hiyo ya Kibaoni- Sitalike ujenzi wake ulitakiwa uwe umefikia asilimia 50 lakini mpaka kufikia sasa unasuasua.

"Barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Kavuu na halmashauri nzima ya Mpimbwe kwa kuwa ni ya kimkakati kwa uchumi wa wana Mpimbwe," alisema Pinda.

Pinda alimwomba Waziri Bashingwa kuitupia jicho la karibu barabara hiyo kutokana na umuhimu wake, lakini pia kuwaokoa wananchi wa jimbo lake kutokana na adha wanayoipata wanapoitumia barabara hiyo.

Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi ni moja ya maeneo ya uzalishaji mazao mbalimbali ya kilimo kama vile mpunga, mahindi, ufuta na alizeti na kukamilika kwa barabara hiyo itakuwa kichocheo kikubwa cha usafirishaji mazao hayo na kuwezesha wananchi kuinuka kiuchumi.

# Wawili wafariki dunia kwa kupigwa na radi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WATU wawili katika Kijiji cha Kigugu, Mvomero mkoani hapa, wamefariki dunia kwa kupigwa na radi usiku, wakiwa ndani ya nyumba wakiangalia mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) hatua ya robo fainali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitokea juzi mwaka huu majira ya usiku katika kijiji hicho.

Mkama alisema watu hao wawili walikuwa sabuleni usiku wakiangalia mashindano ya mpira wa miguu na mvua ilikuwa ikinyesha ikiwa imeambatana na radi.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Juliana Robert (31), mkazi wa Kungwe na Mateso Athanas (35) pia mkazi wa Kungwe wilayani Mvomero.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mkama aliwashauri wananchi kuchukua tahadhari nyakati za mvua zinaponyesha zinazoambatana na radi kwa kuzima umeme na vifaa vingine vya mawasilino ikiwemo simu na televisheni.

Alisema vifaa hivyo kuna uwezekano mkubwa kuingiliana na mawimbi ya radi, kwa kufanya hivyo wakataweza kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza nyakati hizo.

Februari 2, 2024 ilianza michuano ya Afcon hatua ya robo fainali, kwamba majira ya saa 2:00 usiku kulikuwa na mechi kati ya Nigeria dhidi ya timu ya Angola. Katika mechi hiyo, Nigeria iliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Siku hiyo pia majira ya saa 5:00 usiku kulikuwa na mechi nyingine kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) dhidi ya Guinea na DRC iliibuka kidedea kwa ushindi wa mabao 3-1.

# Mzee Mwinyi alazwa, watu wamwombea

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, amelazwa hospitalini akiugua maradhi ya kifua.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi usiku kwa umma na msemaji wa familia, Abdullah Ali Mwinyi, Rais Mstaafu Mwinyi anaendelea kupata matibabu chini ya uangalizi wa karibu wa madaktari.

Pasipo kutaja hospitali aliyolazwa, taarifa hiyo ilieleza kuwa kutokana na ushauri wa madaktari wake, familia imeona ni vyema apate faragha akiwa anapatiwa matibabu.

"Hivyo familia inaiomba jamii kumkumbuka kwenye dua, sala, na maombi," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilisema: "Tunamwomba Mwenyezi Mungu amjaalie shifaa ya haraka mzee wetu pamoja na wagonjwa wengine wote wanaokabiliwa na maradhi mbalimbali".

Tangu kutolewa kwa taarifa hiyo, Watanzania mbalimbali wakiwamo viongozi kupitia akaunti zao za mitandao ya kijamii, walijitokeza kumtakia heri ya afya Rais Mstaafu Mwinyi.

Mmoja wa watu hao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, kupitia akaunti yake ya Instagram aliandika: "Tuungane kumwombea mzee wetu Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili apone haraka. Mwenyezi Mungu ashushe uponyaji na awape maarifa madaktari wetu ili wakomeshe maradhi yanayomkabili."

Mwingine ni aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi, ambaye aliandika: "Mwenyezi Mungu wa rehema akujaalie shufaa upone maradhi yanayokusibu. Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi unazo dua zeu. Amin."

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Afrika Mashariki (EALA), Shyrose Bhanji aliandika: "Mungu akufanyie wepesi baba. Tunakupenda na kukuombea urejee katika afya yako."



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wabunge watambue yawapasayo kutenda sehemu na wakati ufaao

**BUNGE** la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaendelea na mkutano wake wa 18 jijini Dodoma, huku likiwa tayari limepitisha miswada mitatu nyeti iliyokuwa ikivuta hisia za Watanzania wengi. Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kabla ya kupitishwa kwa miswada hiyo, kulikuwa na mijadala mikali iliyotolewa na wabunge iliyofanya serikali kukubaliana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala ambayo ilipokea maoni na kuyachakata kabla ya kuwasilishwa bungeni. Miongoni mwa mambo yaliyokubaliwa ni mwenyekiti na makamu mwenyekiti wa NEC kupitia katika usaili kama wajumbe wengine wa tume kabla ya majina yao kuwasilishwa kwa Rais kwa kuridhiwa na hatimaye kuteuliwa.

Pamoja na mjadala wa miswada hiyo na shughuli zingine za Bunge kama maswali ya kawaida na yale yanayoelekezwa kwa Waziri Mkuu, kuna jambo lililovuta hisia na mijadala kutoka kwa wadau wa siasa. Jambo hilo ni Mbunge wa Momba (CCM), Condester Sichalwe, kutinga na video fupi bungeni inayoonesha baadhi ya wananchi wa jimbo hilo wanavyopata adha ya maji safi na salama, hivyo kutumia maji machafu yanayopatikana kwenye visima vya asili.

Mbunge Sichalwe alisema amefikia hatua hiyo baada ya wizara ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria iliyoahidi kuchimba visima vya dharura lakini hadi sasa hakuna hata tone la maji. Wizara ilieleza Aprili, mwaka jana kuwa Sh. bilioni 9.5 ziliahidiwa kumaliza tatizo la maji katika jimbo hilo lakini hakuna utekelezaji wowote uliofanyika.

Kutokana na kutokutekelezwa kwa ahadi hiyo, alisema anaogopa kwenda jimboni kuwaeleza wananchi wake kwa kuwa ataonekana tapeli. Kwa maneno mengine, wananchi watakosa imani naye, hali itakayomfanya akose kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Hata hivyo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipopewa nafasi, alijibu kwamba kitendo hicho kinaweza kuwakatisha tamaa watendaji kwa kuwa kazi inafanyika katika kutatua kero hiyo jimbo la Momba.

Ni wazi kwamba mbunge alikuwa akiwakilisha kilio cha wananchi wake lakini jambo la kujiuliza ni je, katika eneo hilo hakuna Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) ambao umepewa jukumu la kutekeleza miradi ya maji? Pia ni hatua gani iliyochukuliwa katika ngazi ya halmashauri kwa maana ya baraza la madiwani katika kutatua kero hiyo.

Kama alivyosema mbunge kwamba suala hilo lilifikishwa bungeni mwaka jana, lakini kulikuwa na ulazima gani wa kulirejesha ilhali Waziri anasema katika kuanza kwa kazi hiyo, serikali ilishatoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuanza kutekeleza miradi hiyo?

Licha ya kulalamika, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, awali alijibu kwamba jimbo hilo lina jumla vijiji 72 na mpaka sasa vijiji 30 vinapata huduma ya maji safi na salama kupitia miradi 18 ya maji ya bomba. Sambamba na vijiji hivyo, ilielezwa kuwa kuna utekelezaji wa miradi mingine ya maji katika vijiji 12 ndani ya Momba.

Hatua aliyochukua mbunge ni nzuri na ina mashiko lakini ni vyema wabunge wakajua nini yawapasayo kufanya wawapo bungeni na yale wakiwa katika halmashauri. Ni dhahiri kwamba Sichalwe angepata majibu kama angefuatilia ngazi ya wilaya kupitia RUWASA vinginevyo, kinachoonekana alikuwa akihofia kupoteza ugali wake ifikapo 2025 kwamba hakuna kitu alichokifanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Utoro ni adui wa maendeleo ya elimu, usiwe sehemu ya maisha ya wanafunzi



Na Sabato Kasika

**NI** wiki ya nne imeanza tangu shule zifunguliwe, lakini baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika sekondari za mikoa mbalimbali hawajaripoti shuleni.

Miongoni mwa mikoa hiyo ni Geita, ambayo wanafunzi 7,297 kati ya 8,292 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza hawajaripoti shuleni katika Halmashauri ya Mji wa Geita.

Hayo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe, hiyo ikiwa ni sehemu ya mkoa wa Geita, kwa upande wa mkoa wa Mara, zaidi ya wanafunzi 20, 572 wa kidato cha kwanza hawajaripoti shuleni.

Mkuu wa Mkoa huo, Said Mtanda anafafanua kuwa 52, 784 walichaguliwa kujiunga shule za sekondari mkoani humo, lakini hadi kufikia Januari 17 ni wanafunzi 32, 212, ambao wameripoti shule.

Baada ya kuelezea kwa kifupi, nijadili suala hilo kwamba, utoro shuleni ni adui wa maendeleo ya mwanafunzi, hivyo ingekuwa ni vyema kama utafanyika mkakati wa kujua chanzo kukitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Mkoa wa Mara na sehemu ya mkoa wa Geita, ni wanafunzi 27, 867 ambao hawajaripoti shule, sasa ikiwa hali kama hiyo itakuwa nchi nzima mbona wanafunzi wengi watakuwa wako nyumbani hadi sasa.

**Mkoa wa Mara na sehemu ya mkoa wa Geita, ni wanafunzi 27, 867 ambao hawajaripoti shule, sasa ikiwa hali kama hiyo itakuwa nchi nzima mbona wanafunzi wengi watakuwa wako nyumbani hadi sasa.**

Tanzania Bara ina mikoa 26, iwapo kila mkoa utakuwa na idadi ya wanafunzi watoro kama mkoa wa Mara, maana yake ni kwamba wanafunzi 534, 872 hawapo katika shule walizopangiwa.

Inawezekana wengine wazazi wao wamewapeleka katika shule za kulipia, lakini sidhani kama watakuwa wengi kiasi hicho, bali sehemu kubwa wanaweza kuwa ni watoro.

Serikali imekuwa ikitumia njia ya msako kwa wanafunzi watoro, lakini bado utoro huo umeendelea kuwapo, ninadhani ipo haja ya kubadili mbinu ili kujua chanzo cha tatizo iwe rahisi kulitafutia ufumbuzi.

Ninadhani mbuni mojawapo ni kuwauliza wazazi, walezi na wanafunzi wenyewe kwa nini kunakuwapo utoro ili waeleze sababu, kwani wakati mwingine ni kutojua umuhimu wa elimu, kinaweza kuwa chanzo. Kima

Kama chanzo kitakuwa hicho, basi waelimishwe na wahamasishwe waendelee kisha wachukue hatua, lakini pia kama tatizo ni mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, yaboreshwe na kuwa rafiki kwa wanafunzi.

Si siri kwamba shule za sekondari hasa za vijijini zina changamoto nyingi ikiwamo kuwa mbali na pia ukosefu wa mabweni, huenda vikawa chanzo cha utoro kwa baadhi ya wanafunzi.

Wengine wanaweza kuona kama ni kujitesa kutembea umbali mrefu shule na kukuta mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji si rafiki na pia hakuna chakula na hivyo wanaona ni bora waachane na usumbufu huo.

Mazingira rafiki ya ujifunzaji na ufundishaji, shule kuwa karibu, kuwapo kwa mabweni na pia chakula cha mchana, vinaweza kusaidia kukabiliana na utoro, kwani hivyo ni sehemu ya vivutio kwa wanafunzi.

Lakini katika kundi hilo la watoro, inawezekana wapo ambao wamefaulu bila kujua na kusoma, hivyo hawaoni umuhimu wa kwenda sekondari na kuamua kukaa nyumbani na kuendelea na shughuli nyingine.

Hivi karibuni nilipata kisa cha aina hiyo, Musoma Vijijini mkoani Mara, baada ya mwanafunzi kuwagomea wazazi kwenda kidato cha kwanza akidai hajui amefauluje kwa maelezo kwamba hajui kusoma na kunadika.

Sasa kama hilo lina ukweli ndani yake, inawezekana wapo wanafunzi wa aina hiyo maeneo mbalimbali ya nchi na wanaweza kusababisha kuwapo kwa utoro kila mwaka wa masomo.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# *Sheria mpya kupitishwa sasa lakini mabadiliko ya Katiba bado ni muhimu*



**Pascal Mayalla**

JAPO miswada mitatu ya Sheria ya Uchaguzi, Sheria ya Tume ya Uchaguzi, na Sheria ya Vyama vya Siasa imepitishwa bila kuzingatiwa maoni ya wachache waliotaka kufanyika kwa marekebisho madogo ya katiba, tuendelee kujifunza kuwa watu wa shukrani kwa sheria hizi. Tunapaswa kushukuru kwa kidogo kilichopatikana, wakati tukiendelea kuomba tuletewa kile kikubwa tulichoomba cha mabadiliko madogo ya sheria.

Mtu msafiri mwenye njaa, ambaye alitamani kula pilau au biryani mwisho wa safari yake, na baada ya kufika akaletewa mlo umefunikwa kwa kawa, akajua ni pilau au biriani kuku, mbuzi au ng'ombe, lakini alipofunua akitumaini kukuta pilau au biriani, la haula!, akakutana na ugali maharage, je, atasusa kula?

Atakachofanya ni kula huo ugali maharage na baada ya kula, atamshukuru mwenyeji wake kwa kumkirimu kwa chakula, kisha siku nyingine atamweleza mwenyeji wake kuwa akija safari ijayo, utafurahi zaidi kwa kuandaliwa pilau nyama, pilau kuku au biriani mbuzi.

Hiki ndicho kilichofanyika Bungeni, kwa miaka zaidi ya 30 ya tangu kurejea kwa mfumo wa vyama vingi nchini mwaka 1992. Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, ilikuwa ya chama kimoja, hivyo kulipaswa kufanyika mabadiliko ili tuwe na katiba ya vyama vingi. Hivyo ndivyo tumekuwa tukililia mabadiliko ya Katiba na mabadiliko ya sharia lakini tumepatiwa kidogo, hivyo tushukuru kwa kusema asante, kisha tuendelee kuomba mabadiliko madogo ya katiba.

Mfano mzuri na mfano hai ni Katiba ya Tanzania ya 1977, imenajisiwa kwa kuchomekewa kifungu fulani batili, waliokichomekea kifungu hicho ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT).

Aliyeubaini ubatili huo ni Mahakama Kuu ya Tanzania, aliyeulinda ubatili huo ni Mahakama ya Rufani ya Tanzania, hivyo mpaka sasa katika sheria hii mpya iliyopitishwa, bado upo ndani ya katiba yetu na tusipofanya mabadiliko madogo ya katiba, tutaenda kwenye uchaguzimMkuu wa 2025 bila kuuondoa ubatili huu, ambao tumekuwa tukiendesha uchaguzi wetu wote kila wakati kwa ubatili huu.

Bunge letu limeshehenezwa na wanasheria manguli, wabobezi na wabobevu kuanzia Katibu wa Bunge ni mwanasheria nguli mbobezi na mbobevu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mwanasheria nguli, mbobezi na mbobevu, Waziri wa Sheria ni mwanasheria nguli mbobezi na mbobevu, mawaziri na makatibu wakuu kadhaa nao ni wanasheria waliotopea katika fani hiyo.

Miongoni mwao ni wanasheria waliobobea na wamesoma na kuhitimu vyuo vikuu vyenye heshima kubwa dunia kwenye fani ya sharia kama Yale na Harvard. Wote hawa hawakuona huo ubatili kwenye miswada hiyo.

Bunge letu Tukufu likatunga sheria batili inayokwenda kinyume cha Ibara ya 13 ya Katiba ya JMT na kumpelekea Rais akaitia saini kuwa sheria batili ili ianze kutumika. Wa kulaumiwa kwa ubatili huo si Rais aliyetia saini bali ni wasaidizi wake wanasheria waliompelekea! Kwa hiyo Rais wa JMT hapaswi kulaumiwa, hivyo sheria hii mpya yenye ubatili ule ule, sasa anapelekewa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kuitia saini.

Tuanze na Ibara ya 5 ya Katiba ya JMT inatoa haki kuu ya kwanza ya kidemokrasia, haki ya kupiga kura. Japo haki hii bado imo kwenye katiba yetu, imeingiliwa na kukiukwa na ukosekanaji wa haki ya kuchaguliwa, hivyo Watanzania kuruhusiwa kuwachagua si viongozi wao wanaowapenda kwa uhuru, bali Watanzania wanalazimika kuwachagua viongozi waliopitishwa na chama cha siasa. Huko ni kukiuka nia njema ya mtunga Katiba ya kila Mtanzania anakuwa na haki ya kupiga kura kuchagua kiongozi anayemtaka lakini kwa Tanzania ni kumchagua kiongozi chama kilichowachagulia!

Pia Ibara ya 21 ya Katiba ya JMT imetoa haki kuu ya pili ya msingi ya kila Mtanzania akifikisha umri wa miaka 21, kugombea uongozi toka wa serikali ya mtaa hadi serikali kuu. Ibara ya 39 ya Katiba imeweka umri wa miaka 40 kugombea urais wa JMT. Haki zote hizi, zikaja kuporwa na Ibara ya 67 kumlazimisha mgombea kudhaminiwa na chama cha siasa.

Hii ni haki muhimu iliyotolewa na Katiba, hivyo kitendo cha kuingiza sharti la kudhaminiwa na chama cha siasa ni kinyume cha Katiba. Kwa hiyo sheria hii ibadilishwe ili kukidhi kile ambacho mtunga Katiba ilidhamiria ilipoiweka haki hii,ndani ya katiba yetu, hivyo baada ya mabadiliko hayo ya mlango wa nyuma, kipengele hicho sasa kinasomeka hivi

Ule uhuru uliotolewa na Katiba wa kila mtu kuwa huru kushiriki shughuli za uongozi, kupitia ibara ya 21, umekuja kunyofolewa na ibara ya 39 na 67 (b)(c) kwa kuweka sharti, ili mtu kugombea nafasi yoyote ya uongozi wa umma, ni lazima awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa. Kwa mantiki hiyo, lazima adhaminiwe na chama cha siasa! Haki zinatolewa na ibara moja halafu zinaporwa na ibara nyingine ya katiba hiyo hiyo!

Tanzania tumebarikiwa kumpata Rais mpenda haki na mtenda haki. Rais Samia kwanza zitie saini hizo sheria zilizoko mbele yako zianze kutumika lakini pia tukuombe tu kutumia mamlaka yako kama Rais mtendaji (executive president) kubadili kufanya mabadiliko madogo ya katiba, kwa kutumia hati ya dharura kwa jinsi ile ile ubatili huo ulivyochomekewa ndani ya Katiba yetu ili uchaguzi wa mwaka 2025 uwe huru na wa haki.

**Mungu Mbariki Rais Samia**
**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# *Chifu Bagolole apewe maua au miiba yake*



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

WANASEMA ukiona maharage yanarukaruka kwenye sufuria au chungu motoni, basi ujue yanaanza kuiva. Nchi inarukaruka, imeanza kuiva, tunakaribia kwenye uchaguzi mwaka huu na mwakani.

Kila sehemu hivi sasa watu wanahaha, wakifikiria jinsi ya kuingia au kurejea, wanataka kuchaguliwa na wanajua si kazi rahisi na kama walikuwamo na wakaahidi sasa wanafikiria kama walitimiza.

Wananchi nao walioshika mpini, wanaangalia na kutathmini nani aliahidi nini na amefanya nini na kama anastahili kuendelea au kupisha mwingine kwa nafasi aliyo nayo.

Ngoma kubwa inalilia bungeni ambako kuna waliochaguliwa kwa kutoa ahadi lakini wako waliochaguliwa kwa hila tuna waliochaguliwa kwa matakwa ya watu au mtu fulani.

Wote wako bungeni na wanadai kuwakilisha wananchi 'waliowachagua' mwaka 2020, huku wananchi nao waliwatazama jicho pembe na kuomba siku ifike watamke kupitia masanduku ya kura.

Huu ni wakati ambao mwananchi anatakiwa ajiepushe kudanganywa na wapenda madaraka waishio Tumbo Street, wanaodhani ni haki yao kuchaguliwa na ni haki yao kula bila kunawa. Mambo hayo yanaendana na kufanyika kwa ziara za mtu mmoja mmoja au makundi kujitambulisha au kutambulisha kundi lenye unasaba na anayetaka au watu wanaotaka kuwania kitu fulani.

Tunamshuhudia sasa Chifu Bagolole akizunguka takriban nchi nzima kwa kile anachosema au kinachosemwa ni kujenga kundi lake au chama chake cha siasa kilichomtuma.

Kuna maneno mengi yanatoka vinywani mwa watu kuhusu ziara ya Chifu Bagolole ambaye anadai katumwa na Chifu Hangaya, kupita akisikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Chifu Bagolole naye anaifurahia ziara hiyo akipanda majukwaani akizingirwa na kushangiliwa na wananchi, huku akiwahoji kuhusu kero na kadhia zinazowakabili na yeye kuwaita watendaji kutoka kokote waliko kufika kuzitatua.

Wanaonufaika na ziara hiyo wanamwona kama mkombozi wao, huku walio tofauti naye wakiona ni kama anadhalilisha na kufedhehesha watendaji, lakini pia wakidai anajipa madaraka makubwa isivyotakiwa.

Lakini wanashindwa kuona kwamba Chifu Hangaya anamuunga mkono na nyakati zingine akimpigia simu akiwa majukwaani na kumpongeza kwa analofanya.

Wanaolalamika wanashindwa kusoma alama za nyakati, kwamba nchi inarukaruka na inakaribia kuiva. Hawajui kuwa chama cha Chifu Bagolole kilikuwa kimekaa tenge na hivyo anajaribu kukirejesha mahali pake. Mnaohoji Chifu Bagolole ni nani basi jueni ni Paulo huyu huyu mnayemjua, aliyetikisa Dar es Salaam miaka ya nyuma enzi za Jiwe, baadaye akaingia mitini na sasa kurejea kwa kasi kubwa.

Anaibua kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi sawia. Inadaiwa kuwa anavyofanya anaianika serikali, kwamba haipambani na matatizo ya wananchi mpaka anapofika yeye, ndipo wanapata wasaa wa kuyaanika. Lakini pia kuna maeneo kero hizo ni za miaka nenda rudi na zimekuwa zikirushwarushwa kama mpira na kuacha wananchi wakiendelea kunung'unika. Wananchi wanachotaka si sura ya mtu wala wajihi wake, bali ni kuona matatizo yao yanamalizwa sawia nao wanaendelea na ujenzi wa Taifa lao lakini pia mustakabali wao mwema.

Yawezekana wapo wanaomwona Chifu Bagalole kuwa anatafuta umaarufu au anajijengea uhalali wa kuwa kiongozi wa nchi siku zijazo, lakini hata kama ndivyo ni hiari yake na ya wananchi watakaoamua kama atawafaa au la.

Liwalo na liwe, anachokifanya kinasaidia baadhi ya watu na kinaumiza wengine, lakini la msingi ni kuona wananchi hawateseki huku wakiwa na viongozi wao weledi waliowachagua.

Yawezekana pia Paulo anawasaidia kuona ni nani wa kweli anayeweza kuwasaidia na ni nani longolongo anayejali tumbo lake na si maslahi mapana ya wananchi ambao ndio waajiri. Wako pia wanaohoji kuwa inakuwaje leo Paulo yule aliyekuwapo wakati ule watu wanatekwa na wengine kushambuliwa, leo anapanda jukwaani na kuangua kilio kwa kusikia kuna watu wametoweka bila kujulikana waliko.

Wanashangaa eti ni Chifu Bagalole yule ambaye wakati ule kuna watu walitangazwa kuhusishwa na mihadarati, lakini hakuna hata mmoja aliyepatikana na hatia na badala yake wengine wakapoteza ajira na biashara zao, leo anatetea watu kutendewa haki.

Wanashindwa kuelewa kuwa Chifu Bagalole ni kama aliyebatizwa upya na sasa anajua ni nini uchungu wa familia kupotelewa wapendwa wake bila kujulikana waliko hadi leo, au mtu kushambuliwa na washambuliaji wasiojulikana.

Hao hao wanashindwa kubaini, kwamba ukiwa mchezaji soka ni vigumu kuona kama unafanya makosa bali watazamaji ndio wanaoona kuwa unafanya makosa na sasa Chifu Bagalole hachezi ni mtazamaji na ndiyo sababu anayaona makosa.

Yawezekana kabisa Chifu Bagalole anaisaidia CCM kuona jinsi watendaji wanavyoshindwa kumsaidia Chifu Hangaya, huku pia akisaidia wapinzani kuona udhaifu ndani ya Serikali na kutumia mwanya huo kuipoka kura mwaka huu na mwakani! Sijui atapewa maua au miiba! Siku hazitatudanganya walahi!

# Kamati CCM yampa maagizo mkandarasi

**Na Steven William,** MUHEZA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Muheza mkoani Tanga, imemwagiza mkandarasi anayejenga jengo la Ofisi ya Utawala la Halmashauri ya Muheza kuongeza nguvu kazi ya mafundi pamoja na kufanya kazi usiku na mchana ili akamilishe kazi kwa wakati.

Agizo hilo limetolewa juzi na Katibu wa CCM Wilaya ya Muheza, Simon Leng'ese, alipofanya ukaguzi wa mradi huo katika eneo la Lusanga wilayani hapa.

Ukaguzi huo ni sehemu ya maadhimisho ya chama hicho kutimiza miaka 47, kwa Wilaya ya Muheza yaliyofanyika katika Kata ya Nkumba, kulikoambatana na shughuli ya kufanya usafi wa mazingira.

Akizungumza katika ziara hiyo, Leng'ese aliagiza wasimamizi wa miradi kuhakikisha wanasimamia miradi yote inayoendelea katika halmashauri ili kukamilisha ndani ya muda uliokusudiwa na kuwa chachu kwa wananchi.

Pia aliagiza kuongeza usimamizi wa kutosha katika miradi yote ili iweze kujengwa katika ubora unaotakiwa.

Leng'ese alisema ni lazima miradi yote inayoendelea katika Wilaya ya Muheza ikamilike kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa miradi hiyo na kununua vifaa bora vya ujenzi.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu alimtaka mkandarasi huo kuhakikisha wanajenga jengo hilo kwa ubora zaidi, kwa kuwa mpaka sasa serikali imepeleka fedha shilingi bilioni mbili.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Muheza, Aziza Mshakangoto pamoja na Katibu wa Jumuiya ya Wazazi CCM Wilaya ya Muheza, Hatibu Bakari walisema kamati ya siasa ya wilaya imekuwa na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuitolea maelekezo.

# Wastaafu walia kutopata majibu ya kero

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS wa Umoja wa Wastaafu Tanzania (REAT), Dauda Bilikesi, amesema ni mwaka sasa wanafuatilia pasipo kupata majibu hoja walizoziwasilisha serikalini ikiwamo ya mifuko ya hifadhi ya jamii kugharamia mazishi ya wastaafu wanapofariki dunia.

Hoja nyingine ni pendekezo la kuangaliwa upya kwa kanuni zilizotungwa na waziri kuhusu kikokotoo kwa kuwa uamuzi huo ulifikiwa kwa kukiuka sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alibainisha hayo juzi jijini hapa, alipokuwa akitoa taarifa ya umoja huo kwa wanachama na wastaafu wa chama hicho kuhusu ufuatiliaji wa hoja walizowasilisha serikalini Januari 5, mwaka jana.

"Aprili 5, mwaka jana, Spika wa Bunge alitoa maelekezo kwa viongozi wa REAT kuwasilisha hoja za wastaafu kwenye Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ambapo hoja hizo ziliwasilishwa kwenye kamati hiyo iliyoketi chini ya Mbunge wa Tabora, Aprili 5 mwaka jana," alisema.

Alisema hoja hizo walizoziwasilisha ni pamoja na kima cha chini cha pensheni kuwa sawa na theluthi mbili ya kima cha chini cha mshahara.

Hoja nyingine ni pensheni ya kila mwezi kuendelea kulipwa kwa mwenza wa mstaafu kila mwezi baada ya kifo cha aliyekuwa analipwa pensheni badala ya malipo ya mkupuo ya miezi 36 ambayo hata hivyo hailipwi.

Alisema hoja nyingine ni ushirikishwaji wa wastafu katika masuala ya maendeleo ya nchi na kuundwa kwa kamati ya kushughuikia matatizo ya wastaafu yaliyowasilishwa na Umoja wa Wastaafu Tanzania.

Kadhalika alisema hoja zingine ni utoaji wa hudua bora za afya kwa wastaafu, astaafu wapate bonasi kutokana na faida zinazopatikana kwenye mifuko inapowekeza.

"Ufanyike uboreshwaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii ili iwe na uwezo wa kifedha kutoa huduma kwa wanachama wake kwa serikali kulipa madeni yake kwenye mifuko na ukusanyaji wa michango kutoka serikalini" alisema

Akizungumzia kuhusu ufuatilijai wa majibu ya hoja hizo serikalini, alisema Januari 25 mwaka huu viongozi wa kamati kuu ya REAT walifuatilia kwa Spika wa Bunge na kujulishwa kuwa zinafanyiwa kazi kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Alisema pia umoja huo uliwasilisha hoja za nyongeza kuhusu masula ya wastaafu ikiwemo kilio cha kikokotoo.




Mwendesha Bajaj, Adija Bakari, akiifanyia matengenezo bajaj yake baada ya kuharibika katika eneo la Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waliofanya vizuri kidato cha nne wazawadiwa

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI waliomaliza kidato cha nne kwenye shule ya sekondari St Mary's Mbezi Beach, na kufaulu kwa daraja la kwanza, wamepewa zawadi mbalimbali kama motisha kwa wanafunzi wengine kuendelea kufanya vizuri kitaaluma.

Hafla ya kuwapongeza wanafunzi hao ilifanyika jana kwenye maeneo ya shule hiyo, Mbezi Beach na kuhudhuriwa na wazazi na wanafunzi waliomaliza kidato cha nne.

Zawadi walizopewa wanafunzi hao ni pamoja na fedha taslim, nguo za michezo pamoja na vitabu mbalimbali vya kitaaluma.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Makamu Mkuu wa shule hiyo, Rajab Balele, alisema mwaka 2020 walimu waliahidi kuleta mageuzi makubwa na walipambana usiku na mchana na kufanikiwa kupata matokeo mazuri.

Balele alisema wanafunzi 106 wa shule hiyo walihitimu kidato cha nne mwaka jana na miongoni mwao, wanafunzi 29 walipata daraja la kwanza, daraja la II wanafunzi 35 wanafunzi 13 daraja la tatu na kwamba hakuna aliyepata sifuri.

"Walimu kwa kushirikiana na wanafunzi wamefanyakazi kubwa sana usiku na mchana kuwa wabunifu kufundisha mpaka wanafunzi wengi kufaulu kwa alama za juu.

"Nilipopata matokeo yetu ya kidato cha nne kwa kweli nilichanganyikiwa kwasababu sikuwa natarajia kwamba tutafaulisha kwa kiwango kikubwa namna hii, tulilahidi kufanya vizuri lakini matokeo yamekuwa mazuri sana kuliko nilivyotarajia," alisema.

Balele aliwataka wanafunzi hao wasibweteke na badala yake waendelee kufanya vizuri kwenye elimu ya kidato cha tano na sita ili kupata alama zitakazowawezesha kujiunga na vyuo vikuu bila vikwazo.

"Kuna wakati shule ilikuwa hadi daraja 0 wanafikia wanafunzi 62 lakini kwa sasa hakuna division 0, na daraja la kwanza wameongezeka huu ndo mwaka tumefanikiwa kupata divisheni one nyingi kuliko mwaka wowote.

"Kuna kufaulu na kufaulu sana, kwa hiyo ukiangalia matokeo yetu ya mwaka huu darala la kwanza za kiwango cha juu tumezipata nyingi na huo ndio utakuwa mwendo wetu tutahakikisha hakuna daraka 0 miaka yote na daraja la kwanza zitaendelea kuongezeka," alisema.

Mkuu wa Taaluma wa Shule hiyo, Shadrack Mgaya, alisema wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mashindano mbalimbali ya kitaaluma.

Alisema mafanikio ya wanafunzi yanategemea pembe tatu ambazo ni mwalimu, mwanafunzi na mzazi ambapo kila mmoja anapotimiza wajibu wake matokeo yanakuwa mazuri kama ambayo shule hiyo imepata kwa kidato cha nne.


MAISHA
FEBRUARI 4, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




# MANJANO, KIAZI inavyong'arisha ngozi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | N | D | A | N | I |
| A | | | | K | | N |
| G | | G | A | O | | G |
| E | D | A | | M | E | I |
| N | | M | K | E | | Z |
| D | | B | | | | W |
| O | B | A | M | A | | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

SAA, PAA, SIO, TUI, PISHA, FIMBO, MSASA, INAMA, ONDOSHA, DAFTARI


## AMSHA AKILI








## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO wa miaka sita alimuuliza babake:
MTOTO: Baba, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?
BABA: Mungu alimuumba Nabii Adam na Hawa. Kisha wao wakaanza kuzaa watoto na watoto wakazaa mpaka tukazaliwa sisi. (Mtoto hakuri dhika akamfuata mamake)
MTOTO: Mama, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?
MAMA: Wanasayansi wamesema sisi tulitokana na manyani baadae tukawa binadamu. (Mtoto akarudi kwa baba)
MTOTO: Baba mbona mama anasema sisi tulikuwa manyani mwanzo?Au wanidanganya?
BABA: Mwanangu, mimi nimekuelezea kuhusu ukoo wetu. Mamako amekuelezea kuhusu ukoo wao.

**SWALI**

Samaki aina ya Pweza ana mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kinababa sasa wanaachwa na wake zao kiaina

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Mara nyingi tumekuwa tunashuhudia baadhi ya kinababa wakiwafanyia vituko wake zao kwa ama kuhama kwa muda au kuhama moja kwa moja majumbani mwao na kujichimbia kwenye nyumba ndogo (wake wadogo).

Taswira hiyo imezoeleka sana ndani ya jamii yetu. Lakini ipo taswira nyingine ambayo inachipuka kwa kasi katika miaka ya hivi karibuni ambapo baadhi ya kinamama kwa sababu fulani fulani wanachepuka na kuzihama nyumba zao kwa kuvizia wakidai wanataka kujitegemea.

Kinamama wengi wa aina hii ni wale ambao ama bado wako kazini au wamestaafu na kujizolea mafao ambayo yanawapa kiwewe na kujiona kuwa wanaweza kuishi peke yao bila waume zao na maisha ya uzeeni yakasonga mbele bila vikwazo.

Kinachotokea ni kwamba, kwa zile familia zenye uwezo ambapo baba na mama ni wafanyakazi au wafanyabiashara, ndizo hasa zilizovamiwa na kirusi cha utengano na kuiacha jamii ikizitizama kwa jicho moja kuona mwisho wake.

Nimeeleza hapo juu kwamba kinababa ndio wamekuwa na mchezo wa kuzihama familia hasa za ndoa na kujichimbia nyumba ndogo wanazoita wengine sabuni za roho. Lakini sasa kibao kimegeuka kinababa wanahaha 'mbona wanaachwa kiaina?'

Hivi sasa kinamama wengi wameamua kuingia ulokole wakiamini kuwa ndiyo njia pekee ya kumtumikia Mwenyezi Mungu. Waweza kumkuta mwanamama aliyekuwa mywaji pombe wa kupindukia lakini sasa ameacha. Ukimuuliza kwa nini, jibu "nimeokoka na kuachana na matendo ya shetani".

Wengine wameziacha dini zao za asili (zile walizobatizwa nazo) na kujiunga na makanisa mengine wakiamini kuwa huko kuna wokovu zaidi. Hii sasa ni imani ya mtu na mtu na siyo vema kuingilia mambo haya kwani mahubiri yananukuliwa toka ndani ya Biblia Takatifu. Maandiko yanasisitiza umoja na siyo utengano.

Baadhi ya hawa wanaoingia ulokole, wamekuwa na vituko majumbani mwao ikiwa ni pamoja na kuhama chumba cha ndoa na ama kulala chumba cha watoto au kujiamulia chumba kingine kama nyumba ni kubwa. Kwa nini, eti ameokoka hataki kusumbuliwa tena uzeeni.

Wako waliojitenga kwa namna hii baada ya kugundua kuwa mume si mwaminifu na pengine alishapata tetesi au ushahidi kuhusu mahusiano ya nje ya ndoa. Akijiridhisha, basi taratibu huchepuka kuepusha shari.

Lakini kuna kujitenga kwingine ambako ndio hasa kiini cha makala haya. Wapo kinamama wasomi, waliokuwa na kazi nzuri, walioishi ndani ya ndoa kwa raha, tena miaka mingi, wakapata watoto, kazi nzuri, lakini wanaamua kuhama chumba cha ndoa na kwenda kujenga maskani mengine.

Kiumri, kinamama hawa ni watu wazima sana. Kwa mfano anapokuwa amefikisha zaidi ya miaka 60, kisha anaamua kwenda kujenga nyumba yake kwingine na kuhama mji wake wa ndoa, siyo maamuzi magumu hayo?

Na baadhi wanaochukua maamuzi haya inawezekana hawajagombana na waume zao, au pengine upo ugomvi wa kitambo lakini unaendelea kimya kimya (huwezi kujua nyumba za watu) kwani masuala ya ndoa ni mtihani mkubwa.

Wengine ni kiburi tu, eti amestaafu, kapata kiinua mgongo chake kilichoshiba, kinamzuzua na kwenda kununua kiwanja, kisha kujenga nyumba yake, tena bila kumshirikisha baba watoto. Ukiona mtu anachukua maamuzi ya aina hii, ujue amemchoka mwenzake ila tu anashindwa kuweka bayana hisia zake. Au siyo msomaji wangu?

Inapotokea jambo kama hili, kinababa katika nyumba husika huanza kuhaha na kujiuliza mara mbili mbili kulikoni sishirikishwi katika mipango ya aina hii? Na kinamama wanaochukua maamuzi ya aina hii siyo kwamba nyumba ya ndoa ni mbaya, la hasha. Wengine wanaishi kwenye mabangaluu (nyumba za kifahari) lakini bado wanaamua kuziacha na kwenda kuanza maisha kwingine japo ni katika dakika za majeruhi. Wameshapata watoto na wajukuu, kwa nini watengane?

Jambo hili la baadhi ya kinamama wanazihama nyumba zao na kwenda kuishi kivyao, nililinasa hivi majuzi kinamama wawili wakibishana kuhusu mwenzao aliyejenga nyumba yake maeneo ya Kiboriloni, huko Moshi na mwezi uliopita amehamia. Lakini hadi anakamilisha nyumba hiyo hakuwahi kumjulisha mumewe.

***Msomaji, ndoa huanza vizuri lakini nyingi huishia vibaya. Maisha ndivyo Yalivyo. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# 'Tumepigwa kitu kizito ukatili wa kijinsia uchaguzi mkuu'

KIOO kinachomsaidia dereva kutazama mbele ni kikubwa kuliko vioo viwili vya pembeni vinavyomsaidia kuangalia nyuma.

Tumia nguvu nyingi kuangalia unakokwenda kuliko ulikotoka. Kama nyuma pangelikuwa muhimu, labda Mwenyezi Mungu angetuwekea macho kisogoni.

Najua kwamba sina maneno matamu ninapoongelea mambo magumu. Hakuna ubishi kwamba wale ndugu zetu wanaotumia majukwaa ya kisiasa kufanya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wagombea wanawake au hata wanaume, tumepigwa kitu kizito.

Hata hivyo, siko vizuri kwenye kupamba na kuwapendeza watu kwa hoja yangu, ambayo nataka kuizungumza hapa, hasa ninapojaribu kupamba mambo kwa maneno bandia, sauti yangu inafunga.

Kwa siku nne mfululizo mwanzoni mwa juma hili, Bunge lilijadili miswada mitatu, ambayo inagusa mioyo ya Watanzania, demokrasia, utu na haki.

Miswada hiyo ni ule Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, yote ya mwaka 2023.

Kupitishwa kwa miswada hiyo, kwangu mimi dhamira yangu iko safi kabisa, kwa jicho langu la kitaaluma. Kwa nini nasema hivyo!

Kuanzishwa kwa kosa la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023, ni hatua muhimu kwa ustawi wa jamii yetu.

Najua, nitaamsha hisia na hasira za wengi ambao hawakubaliani na jambo hili kwa mtazamo wa kifeministi au kwa sura ya kisiasa.

Wabunge wengi waliochangia mjadala huo, hasa wanawake wanadai kudhalilishwa katika uchaguzi uliopita. Hili lina ukweli na waliokuwa na jukwaa la kuibua hoja hizi za unyanyasaji na ukatili wa kijinsia ni vyombo vya habari, lakini mengi hatukuyajua.

Ili kudhibiti vitendo hivyo wakati wa uchaguzi mkuu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, imependekeza kuongeza kosa hilo kwa kuwa vitendo hivyo vinafifisha jitihada za kitaifa kufikia usawa wa malengo ya uwiano wa 50/50 katika uongozi.

Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango Malecela (CCM), alisema anaamini sheria inayotungwa hivi sasa, inakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo hilo.

Namnukuu, "Mimi ni mhanga, ni Mbunge wa Jimbo mwanamke. Nimeanza kugombea jimbo tangu mwaka 2005, nakutana na haya mambo ambayo wengi wanayachukulia ni madogo, la hasha! manyanyaso ni makubwa sana wakati tunapogombea.

"Kwa nini lichukuliwe kwamba ni kosa la uchaguzi. Mwaka 2005, wiki ya pili nagombea uchaguzi Jimbo la Same Mashariki, japo kuna vitu viwili duniani vya kawaida, kupendwa na kuchukiwa hakuna cha ajabu."

Anasema wakati wakiwa katika kampeni za uchaguzi mkuu, mgombea mwenzake alisimama jukwaani na kuingia ndani ya ndoa yangu. Kwa hiyo akawa ananifedhhesha, ananikatili; akasema mambo mazito.

"Mwenzangu aliamua kuniacha, licha ya kuwa bado alikuwa ananipenda. Hivyo, aliponikuta napigia pasi ili niende kanisani, akaichukua akanichoma nayo mgongoni, ikaondoka na nyama.

"Wanawake tunateseka, msidhani hawa wanawake hapa ndani hawataki kugombea majimbo, wanataka lakini wana hofu ya kuogopa haya manyanyaso, wote wana uwezo hivyo suala la unyanyasaji msilichukue kwa udogo serikali."

Kutokana na madhila hayo ya uchaguzi, Mbunge huyo aliitaka serikali kulitazama kwa jicho la karibu, kwa kuangalia viwanja vya mikutano kuwa na amani, akitaka unyanyasaji wa kijinsia liwe kosa la uchaguzi.

"Niliambiwa na nyonyo moja." Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, akichangia mjadala huo alisema, unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake wanapogombea ni mkubwa, huku akifichua siri ya yeye kutukanwa kwa kuambiwa ana nyonyo moja na aliambiwa na viongozi.

Mwingine akasema aliambiwa hana mume. Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu, alisema wakati wagombea kuna mtu alimtukana Iringa, akisema anachaguliwaje kuwa Mbunge wakati hana mume.

Hata hivyo akasema: "Mwanamke ukitukanwa unafundishwa vita, tusilale mimi nimeshaonyesha njia, unalia nini? Simama maana tumepata fursa sawa twende tukagombee, tuitete nchi."

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



ILIKUWA siku ya furaha na nderemo kwa familia ya Kuboja baada ya kumfanyia hafla ya kumuaga binti yao Joyce Kuboja iliyofanyika katika ukumbi wa Gedeko mjini Geita Januari 30, mwaka huu.







MITINDO



# GAUNI LA HARIRI

## mwonekano wa kushangaza

MAGAUNI ya vitambaa vya hariri yamedumu kwa muda mrefu na yanaendelea kutamba katika majukwaa ya mitindo duniani.

Nguo hizi ambazo awali zilikuwa zikivaliwa na familia tajiri na hasa zile za kifalme, zimeanza kutumika katika nchi ya Ugiriki ya kale lakini hadi leo limebaki kuwa vazi pendwa kwa kila mwanamke anayehitaji kuwa nadhifu.

Awali magauni haya yalitengenezwa kuwa marefu na shingo ya umbo la V ili kumpa nafasi mwanamke kuonyesha urembo wake wa shingo na kifua.

Hata hivyo, wabunifu wa mavazi walifanya kazi kubwa kubadilisha mitindo ya nguo hizi kwa ajili ya kuwavutia watumiaji kila siku.

Hata hivyo, mitindo mingi ya magauni ya aina hii yanayovaliwa katika sherehe mbalimbali bado yanashabihana kwa karibu na ile ya kale ya Kigiriki.

Mwanamke anayevaa gauni refu la hariri anaonekana nadhifu zaidi, ana uwezo wa kifedha na mwenye mamlaka.

Kitu cha kushangaza nguo za hariri hazichagui aina ya viatu, lakini viatu vyenye visigino virefu na vifupi huwa nzuri zaidi kutumia.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# MANJANO, KIAZI inavyong'arisha ngozi

MARA nyingi ngozi nyeusi kwenye kiwiko cha mkono au goti husababishwa na mkusanyiko wa seli zilizokufa kutokana na msuguano sehemu hizo.

Kawaida sehemu hizo huwa kavu na hazina uwezo wa kutoa mafuta kama viungo vingine na hivyo zinahitaji kutunzwa na kufanywa kuwa safi.

**Kiazi**

Kiazi kina kimeng'enya ambacho kinasemekana kuwa na uwezo mkubwa wa kundoa weusi kwenye ngozi bila ya kuongeza chochote.

Ukikikata na kukipaka kwenye ngozi yako hasa maeneo ya kiwiko na goti kwa dakika 15 hivi na kisha osha kwa kutumia maji yenye joto kiasi.

Zoezi hili ukirudia siku kadhaa itaifanya ngozi yako kuwa nyororo na kusaidia kuondoa weusi.

**Manjano na Maziwa**

Kabla ya kupaka kwenye ngozi yako unatakiwa kuchanganya manjano yako au Turmeric na maziwa ili kuwa na mchanganyiko bora.

Wataalamu wa masuala ya ngozi wanasema njano ina uwezo mkubwa sana wa kuondoa seli za ngozi zilizokufa hasa katika sehemu za goti na kisugudi.

Manjano pia ina uwezo mkubwa wa kupambana na madini ya melanin ambayo ndio chanzo cha ngozi kuwa nyeusi hasa katika maeneo niliyotaja.


Baada ya kuupaka mchanganyiko wako kwenye goti au kiwiko kaa kwa nusu saa na baadae osha kwa maji yenye joto kiasi.

Rudia kufanya hivi kila siku kwa muda wa wiki au zaidi na bila shaka utapata matokeo mazuri.

Baada ya kuoga, unatakiwa kuupaka mwili wako mafuta hayo hasa maeneo unayohisi ni meusi na yanahitaji kufanywa kuwa angavu.

**Asali na limao**

Asali wanasema waliowahi kuutumia mchanganyiko wa asali na limao kuwa bora zaidi katika kuifanya ngozi yako kuwa nyororo hasa katika maeneo yenye ngozi iliyokauka na seli zilizokufa.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya limao na karoti

KINYWAJI cha juisi ya limao ya karoti ni kizuri kwa ajili ya afya bora katika mwili wa binadamu. Kutengenezwa kwake ni haraka zaidi ukiwa na matunda ya limao, karoti na tufaa.

Juisi hii inafaa kutumika kama kifungua kinywa wakati wa asubuhi au kiburudisho.

Fuata hatua zifuatazo, ili ujifunze jinsi ya kutengeneza juisi hii ya limao ya karoti.

Mahitaji

Malimao mawili, ma apple mawili, karoti kubwa moja, nusu kikombe cha maji, sukari kadiri ya mahitaji yako.

Chukua mashine ya kusaga matunda, weka kwenye hiyo mashine ya kusaga karoti, limao, tufaa (apple), maji, pamoja na sukari, kisha saga hadi utakapoona mchanganyiko umesagika vizuri.

Chuja juisi kwa kutumia chujio, kisha iweke kwenye friji ili ipate baridi kabla ya kunywa.

Unaweza kuongeza maji kwenye juisi hii kadiri upendavyo, endapo utaona maji yaliyomo katika juisi hii ni kidogo.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Tambua namna ya kuepuka magonjwa yanayoathiri nyumba

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo kuathirika, ni vyema ubunifu wake ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Deodatus Kwivilo, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Kwivilo anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipokufanyiwa ubunifu mzuri huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia.

Kwamba mara nyingi hutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.

Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji, na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba ili kuepuka athari baadaye.

"Maeneo mengi ya pwani majengo mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchemu na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.

"Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyopo chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizopo kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine, anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta," anasisitiza.

DONDOO

## Yatumie vizuri madirisha yako

Na Restuta James

JE, umewahi kutamani kuwa na sehemu ndogo ya kustarehe, kupata kikombe cha kawaha, glasi ya juisi au kufanya kazi kwenye kompyuta?

Kama unafikiria kujenga nyumba mpya au kukarabati nyumba yako basi zingatia namna ya kutumia madirisha yako kwa kuongeza kitu cha tofauti kitakachokufanya ufurahi uwapo nyumbani kwako.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza namna bora ya kubuni madirisha ya kisasa yatakayokupa nafasi ya kuongeza nakshi zaidi.

Kwa maeneo yenye joto na mbu kama Dar es Salaam, inashauriwa kuwa mwenye nyumba achague dirisha moja au machache ya kuboresha matumizi.

Mtaalamu Lucy Goldberg, anasema unaweza kujengea kimeza kidogo kwenye dirisha ili kupata nafasi ya kupumzika pale unapohitaji mwanga mwingi hasa kwa wanaotumia kompyuta.

Anasema kama dirisha ni kubwa, ukishajenga meza, badala ya kiti cha kukalia unaweza kuweka kibenchi ambacho kitafaa kulala ikiwa utataka kupumzika eneo hilo.

Anasema unaweza kutumia nafasi hiyo ya dirisha kuweka mito, kitabu upendacho au ua.


"Ni eneo zuri la kufurahia mwanga wa jua na mandhari ya nje," anasema.

**DONDOO**


Viti vya dirishani vinafaa kutumia kama ofisi yako ya nyumbani.

Inafaa kuwekwa vitu vichache kama kitabu, kompyuta, ua, mto na kikombe au glasi.

Ongeza ukisasa na uzamani kwenye eneo hili, tumia zaidi mbao.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
ALIYESEMA 'ASIYE NA NDEVU SANAM!' HATUJAMTUMA NA MKIMUONA MLETENI NIMSUTE KWA UCHOCHEZI.
KWELI SIASA NI 'SI-HASA!' HA HAA
JUDO, KARETI, KUMFUU NA NDONDI VYOTE NIMEFUZU... SASA NAMBIE KAMA YULE MLEVI ALIYENIPIGA NIKAZIMIA 'KAJA TENA? NIJIFICHE MAPEMA SITAKI KESI MIE SINA MBIO
HUTAKI KESI AU HUTAKI KUFA?
HAIWEZEKANI ETI' NIMEMNYWESHA ALAFU WEWE UJITWISHE WAKATI NA WEWE NIMEKUNYWESHA UNANIONA POYOYO!
NISHUKURU MIMI NI JASIRI SANA NAVOKUJUA WEWE LEO LEO TUNGEKUZIKA! BILA AIBU JANAMKE ASUBUHI ASUBUHI LINANIPA USHAURI NASAHA!
'KAPIGA CHABO' SIMU YA MKEWE MESEJI YA KWANZA HAKUIMALIZA 'KAZIMIKA!'
KILANGA KOMO!
RAHA YA BARUA UWE HUJUI KUSOMA KABISA UNAPEPESA HUKU UNATIA NA MADOIDO
UNA'HOFU SANA YA MUNGU HADI NAKUOGOPA... UMENIFUMANIA 'GESTI NA GOMA' UMEKUWA MPOLE TUNARUDI HOMU' KAMA TUNATOKA KUOANA LEO!
'JISHAUE' TU
UMEKATA MGUU UKWENI KWANI WAZAZI WANGU WAMEKUFANYA NINI?
NILIAMBIWA NIKAE CHINI NIMPISHE MUME WA MDOGO'AKO AKAE KAJA NA BENZI MIMI NA DALADALA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SIO MAISHA TU HATA SIKIO UNATOBOA....

## HABARI KIMATAIFA



Rais wa Marekani Joe Baiden, akishiriki mapokezi ya miili ya wanajeshi watatu waliokufa katika shambulio lililofanywa katika kambi yake nchini Jordan wiki iliyopita. **PICHA: AFP**

## KISASI CHA MAREKANI CHATIKISA

# Ndege zatumia dk 30 kupiga Iraq, Syria

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetangaza kujibu mapigo kwa kushambulia maeneo 85 ndani ya nchi za Iraq na Syria na kuua watu 16 na kuwajeruhi 20.

Maofisa wa Marekani walisema jana kwamba mashambulizi hayo wanaamini kuwa yamefanikiwa, lakini bado wanatathmini uharibifu uliotokana na tukio hilo.

Mashambulizi hayo ya kulipiza kisasi yanafuatia tukio la ndege isiyo na rubani kulenga kambi ya kijeshi ya Marekani huko Jordan, na kusababisha vifo vya wanajeshi watatu na kujeruhi 20.

Walifafanua kuwa maeneo hayo saba yalishambuliwa, manne yako nchini Syria na matatu Iraq.

Katika maeneo hayo walengwa 85 walikuwa watu binafsi, ikiwa ni pamoja na vikundi vinavyohusishwa na kuungwa mkono na Jeshi la Walinzi la Revolutionary Guard la Iran.

Baada ya shambulio hilo, maofisa hao walirudia kusema kwamba haitafuti mzozo kati yake na Iran.

Walisema kuwa mashambulizi hayo ya usiku wa kuamkia jana yalilenga kudhoofisha uwezo wa kijeshi na kukomesha shambulio dhidi ya kambi za Marekani katika eneo hilo.

Waliongeza kwamba ndege zote za Marekani zilizohusika katika mashambulizi hayo zimetoka katika maeneo hatari.

Ndege hizo zilitumia silaha 125 kwa muda wa dakika 30 pekee.

Ofisa mkuu wa Marekani alieleza kuwa mashambulizi hayo hayataisha bali yataendelea.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani Joe Biden ametoa taarifa kuhusu mashambulizi hayo ya kulipiza kisasi kwa kuonya hakuna yeyote atakayeachwa kama atamdhuru Mmarekani.

"Leo mchana, kwa maelekezo yangu, vikosi vya kijeshi vya Marekani vilishambulia vituo vya Iraq na Syria ambavyoJeshi la Ulinzi la Iran la Revolutionary Guards Corps (IRGC) na wanamgambo washirika hutumia kushambulia vikosi vya Marekani," alisema.

Aliongeza kuwa hapo awali alihudhuria kupokea miili ya wanajeshi waliokufa na kuwaita kuwa majasiri na kisha alizungumza na familia zao.

"Hatua yetu imeanza leo (jana). Jibizo hili litaendelea katika nyakati na maeneo tunayochagua, Marekani haitafuti mzozo katika Mashariki ya Kati au popote pengine duniani lakini anatoa onyo," Alisema.

Aliongeza"Wacha wale wote ambao wanatafuta kutudhuru wajue hili:, mkimdhuru Mmarekani, tutajibu."

Hata hivyo, msemaji wa waziri mkuu wa Iraq alieleza mshambulizi ya Marekani yaliyofanywa katika ardhi yake ni ukiukaji wa uhuru wa nchi yake.

Kulingana na shirika la habari la AFP, msemaji huyo Jenerali Yehia Rasool, alisema mashambulizi hayo yataleta athari mbaya kwa usalama na uthabiti wa Iraq na eneo zima la kikanda.

Baadae taarifa zilizotolewa na msemaji wa serikali ya Iraq Bassem al-Awadi, alidai kwamba mashambulizi hayo yamepiga maeneo katika mikoa ya Akashat na Al-Qaim, ikiwamo maeneo ambako vikosi vya usalama vya nchi hiyo vimepiga kambi.

Alisema tukio hilo limewasikitisha kutokana na kusababisha vifo vya raia 16 na wengine 23 wamejeruhiwa ambao hawana hatia.

Awali Marekani iliapa kulipiza kisasi na kudai kwamba shambulio la wiki iliyopita dhidi ya kambi yake ya kijeshi lilifanywa na kundi la Islamic Resistance la nchini Iraq, ambalo ni muungano wa wapiganaji wanaoiunga mkono Iran.

Kundi hilo linapinga Marekani kuiunga mkono Israel ambayo inaendelea kupigana na wanamgambo wa Hamasi katika Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo kundi hilo halijadai kuhusika na shambulio hilo na serikali ya Iran pia imekana kuhusika kwa namna yoyote katika shambulio hilo.

Hata hivyo, juzi Ikulu ya Marekani ya White House ilisema nchi yake iliionya serikali ya Iraq kabla ya shambulizi.

Serikali ya Iraq ilikataa madai ya kwamba kumekuwepo na ubadilishanaji wa taarifa na Marekani kabla ya tukio hilo.

Katika hatua nyingine, Iran imelaani mashambulizi hayo ya anga yaliyofanywa na ndege za kijeshi za Marekani nchini Iraq na Syria ikieleza ni kosa la kimkakati.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Nasser Kanani, alisema katika taarifa yake kwamba shambulio la juzi usiku dhidi ya Syria na Iraq ni kosa lingine la kimkakati la serikali ya Marekani, ambalo halitakuwa na matokeo yoyote zaidi ya kuzidisha hali ya wasiwasi na ukosefu wa utulivu wa kikanda.

Alisema Marekani imefanya ukiukaji wa kimamlaka ya nchi za Iraq na Syria, sheria za kimataifa na katiba ya Umoja wa Mataifa".

Jeshi la Marekani pia limekuwa likifanya mashambulizi ya anga dhidi ya waasi wa Kihuthi wa Yemen wanaoungwa mkono na Iran kutokana na mashambulizi dhidi ya meli za kimataifa.

**BBC, DW**

## Watoto 17,000 Gaza hawana wazazi

**GAZA,** PALESTINA

SHIRIKA la kuhudumia watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), limesema watoto wapatao 17,000 wa Kipalestina wanaishi bila wazazi wao au ndugu katika Ukanda Gaza.

Shirika hilo lilisema idadi hiyo ya watoto waliokosa wazazi na ndugu inatokana na mapigano makali yanayoendelea katika eneo hilo kati ya jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas.

Idadi ya watu waliokufa Gaza imefikia 27,131, wengi wao wakiwa wanawake, watoto au vijana, huku 66,287 wakiwa wamejeruhiwa tangu vita hiyo ianze Oktoba 7, mwaka jana.

Msemaji wa UNCEF katika kanda hiyo, Jonathan Crickx, alisema wazazi wa watoto hao watakuwa wameuawa, kujeruhiwa au walilazimishwa kuhamia sehemu nyingine.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani Annalena Baerbock, aliionya Israel dhidi ya kutanua operesheni yake katika mji wa Rafah, kusini mwa Gaza, na kusema hatua hiyo haitakuwa na uhalali wowote.

Waziri Baerbock alisema Ujerumani na Marekani zimeweka wazi kwa Israel kwamba wakazi wa Gaza hawawezi kuondoshwa kwenye maeneo yao.

Kauli hiyo imefuatia ripoti zilizomnukuu waziri wa ulinzi wa Israel, Yoav Galant, akisema kwamba watatanua operesheni hadi Rafah kuzikabili brigedi za Hamas katika eneo hilo la mpaka na nchi ya Misri.

**DW**

SAFU

MAKALA

# HATARI YA VIJANA KUTOSHIRIKI KIKAMILIFU SHUGHULI ZA KISIASA



Na Magabilo Masambu

**Vijana kutoshiriki katika shughuli za siasa, si hasara tu kwa vyama vya upinzani bali hata chama tawala. Madhara yameshaanza kuonekana pale vyama vinapofanya mikutano. Vijana wengi hawajitokezi na hiyo si ishala nzuri. Taasisi za elimu kama vyuo vikuu ambazo zilikuwa kama jiko la kupika viongozi, leo hii vijana katika taasisi hizo hawashiriki kikamilifu katika makongamano mbalimbali kama ilivyokuwa zamani. Hapo lazima tuone kuna tatizo na pengine litafutiwe dawa.**

VIJANA ndiyo taifa la kesho. Wazee na viongozi wa leo walikuwa vijana miaka iliyopita, kwa hiyo walikuwa vijana kabla ya kuwa wazee japo kuna wakati maisha yanaweza kumfanya kijana akaonekana mzee na mzee akaonekana kijana kwa mwonekano wa nje na ndani.

Mara kadhaa nimesikia baadhi ya wanasiasa wazee wakiwataka vijana kutojihusisha na siasa na kwamba siasa ni kupoteza muda. Wanaosema hayo wako kwenye siasa toka ujana wao na hawajawahi kuona kama wanapoteza muda na kujaribu kutafuta kazi zingine ambazo si za kupoteza muda. Jambo hili linanipa wasiwasi juu ya wazee wajao, watakuwa wazee na viongozi wa namna gani katika siasa, ikiwa vijana wanaambiwa siasa ni kupoteza muda.

Tutakubaliana kwamba siasa ni maisha na maisha ni siasa. Hakuna jambo linafanyika kwenye dunia hii bila kuhusika na siasa. Uwe unafanya biashara, kilimo, ufugaji, msomi na kadhalika lazima siasa inahusika kwa sababu uamuzi wa ambo yote unategemea viongozi wa kisiasa. Kwa hiyo jaribio lolote la kuwataka vijana kutojihusisha na siasa ni kujaribu kuyakataa maisha yao wenyewe.

Kuna wakati walioko madarakani wanaweza kuona ni jambo zuri na la afya kuwa na vijana makondoo wasiojua kuhoji, wasiouliza chochote kuhusu siasa au maisha yao lakini athari zake kwa taifa huko mbeleni ni kubwa. Katika nyakati hizi za mfumo wa vyama vingi, vijana wanaokuwa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za siasa kwenye vyama vyao, watakuwa na ujasiri wa kulitetea taifa wanapopata nafasi ya madaraka serikalini. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kushirikishwa na wao kushiriki vyema katika masuala ya kisiasa.

Vijana kutoshiriki katika shughuli za siasa, si hasara tu kwa vyama vya upinzani bali hata chama tawala. Madhara yameshaanza kuonekana pale vyama vinapofanya mikutano. Vijana wengi hawajitokezi na hiyo si ishala nzuri. Taasisi za elimu kama vyuo vikuu ambazo zilikuwa kama jiko la kupika viongozi, leo hii vijana katika taasisi hizo hawashiriki kikamilifu katika makongamano mbalimbali kama ilivyokuwa zamani. Hapo lazima tuone kuna tatizo na pengine litafutiwe dawa.

Utaratibu wa kutumia vitisho kwa vijana wenye mawazo mbadala au yasiyokubaliana na utawala katika taasisi mbalimbali za elimu kutoka shule za msingi mpaka vyuo vikuu, haujengi vijana shupavu kwenye taifa badala yake unajenga vijana waoga wasiokuwa wabunifu kwa sababu tayari wanakuwa na uoga wa kuanzisha jambo lolote. Kwa kujengwa hofu, vijana wanakuwa na mawazo tegemezi. Kila wanachofikiria kufanya wanahisi watakosea na wanahitaji maelekezo kutoka kwa mtu fulani.

Baada ya kipindi fulani cha siasa za nchi yetu, sasa naona tumeanza vizuri pengine mwelekeo huu utaturudisha katika siasa za wakati wa awamu ya nne ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati ambao tuliona uhusika wa vijana wengi katika siasa za Tanzania. Ndio wakati ambao bunge lilikuwa na mvuto kwa Watanzania, wananchi waliacha shughuli zao nyakati za vipindi vya bunge na kuwenda kufuatilia. Ni wakati ambao Watanzania wengi walikuwa wanajitokeza kwenye mikutano ya vyama vya siasa. Siasa za upinzani zilipamba moto na ni kiu yangu nione kipindi kama hicho tena maana ni afya kwa taifa kwa kuwa wananchi wataanza kufuatilia mambo ya msingi yanayoathiri maisha yao ya kila siku.

Nazikumbuka siasa za Arusha, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam pamoja na kuwa na mwitikio mkubwa wa majukwaani kwa kipindi hicho, pia kuliambatana ufichuzi wa masakata ya ufisadi wa fedha za umma. Wako watu walijiuzulu wengine walichukuliwa hatua za kisheria. Yote hayo yalisababishwa na elimu ya uraia kwa wananchi iliyotolewa na vyama vya siasa.

Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba tuwape moyo vijana wa kujiusisha na siasa za nchi yetu ili kujenga ujasiri katika siasa bila kutazama ni vijana wa chama gani. Tusiwafanye waione siasa kama mchezo mchafu kama wengine wanavyoamini bali wajue siasa inaamua maisha yetu sote na ni jambo tunalotakiwa kulipa uzito unaostahili.

Tunatengeneza tatizo halafu tunageuka kuwalaumu vijana tena. Yaani wakitaka kueleza kuhusu masuala yanayowahusu, tunatumia mabavu kuwanyamazisha halafu baadaye wakiwa wanashindwa kujieleza tunasema vijana wa siku hizi hata kujieleza hawawezi na wamefika vyuo vikuu. Nadhani tunawaonea tuwape nafasi ya kujenga ujasiri wa kuhoji wakiwa katika ngazi za chini kabisa, kuanzia kwenye familia na baadaye shuleni wakijenga utamaduni huo tutapata wasomi wanaojua kujitetea na kulitetea Taifa bila woga wowote, tuwajenge vijana tulijenge Taifa la kesho.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es Salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Viko vitu vya kupenda lakini si mke wa mtu*



Na Adam Fungamwango

KUMPENDA mke wa rafiki yako kweli ni hatari, viko vitu vya kupenda lakini vingine vina madhara, oooh moyo utakupeleka kaburini."

Hicho ni kiitikio cha wimbo uitwao, 'Ushinde moyo wako', uliopigwa na OTTU Jazz, wana wa Msondo Ngoma, utunzi wake marehemu, Tx Moshi William.

Wimbo huu ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1990, lakini maana na maudhui yake yataishi milele, dahari hadi mwisho wa dunia hii.

Unawaasa watu wenye tabia ya kupenda au kutongoza wake za wake za watu. Wengine wanakwenda mbali zaidi wanawachukua mpaka wake za rafiki zao.

Kama Tx Moshi alivyobainisha hapo kuwa kitu hicho ni cha hatari kwa sababu inawezekana kabisa kinaweza kumpeleka mtu kaburini.

Ndiyo maana wapo waliobainisha kuwa mke wa mtu ni sumu. Maana yake mwenyewe akigundua anaweza kufanya chochote kinachoweza kuhatarisha maisha yake mwenyewe, mkewe au yule aliyefanya kitendo hicho.

Na kitu kama hicho hakiwezi kutafsiriwa vyovyote vile zaidi ya tamaa na ugomvi, kwani wanawake waliojaa katika dunia hii ya Mungu leo kwenda kuchukua mwanamke ambaye ameolewa tayari au mke wa mtu unayemfahamu?

Vitu kama hivi vimetokea sana kwenye jamii na tumeshuhudia kusababisha matatizo makubwa kwa wahusika na hata jamii kwa ujumla.

Kwanza kabisa, mwenyewe akijua anaweza kuchukua uamuzi ya kujimaliza mwenyewe. WaKo ambao hawana uvumilivu hata chembe, wao wanaamua kujidhuru.

Wengine hawana tabu, wao wanatoa talaka tu. Unaweza ukadhani labda hii ni afadhali kwa sababu kunakuwa hakuna maafa, lakini athari zake ni kwamba mume na mke wanaachana kwa sababu ya mpuuzi fulani, mwanamke anahangaika kwa sababu amedanganya na kutelekezwa, lakini pia kama wana watoto pia wanaanza kuteseka kwa kukosa malezi mema.

Mbaya zaidi kule wale wenye visasi. Asipomfanyizia mkewe, atafanya kila njia kumfanyizia yoyote aliyefanya kitendo hicho kwa mkewe.

Tumeshuhudia watu wakifanyiwa vitendo vibaya, wengine wakitekwa, wapo wanaouawa na hii yote ni kwa sababu ya visasi vinavyosababisha na mambo hayo.

Waswahili wana msemo wao, 'cheza na mtu, usicheze na mke wa mtu.' Hawatanii, wanamaanisha kweli.

Hivi majuzi tu tumesikia mtu mmoja amehukumiwa kwa kuua watu saba wa familia moja. Kisa alikwenda kulipa kisasi cha kumuua mmoja wa watu wa familia hiyo kwa madai ya kuwa anatembea na mkewe.

Kilichotokea ni kwamba alikuwa anaua wengine kwa ajili ya kupoteza ushahidi, kwani baadhi walimuona na wengine walikuwa anapiga kelele. Ni jambo la kusikitisha sana.

Aliyeua hakufanya vyema na aliyeuawa naye 'alizingua', kutembea mke wa mwenzake. Matokeo yake wamesababisha vifo vya watu wasiohusika kabisa.

Si vizuri kama ukipatwa na jambo hilo kulipiza kisasi badala yake vipo vyombo vya sheria kwa ajili ya kufuata mkondo wake. Lakini wenye tabia hii wanatakiwa waache kwa sababu wanajiweka kwenye hatari zaidi kuliko furaha ya muda mfupi wanayoipata.

Ukisoma mashairi ya wimbo wa Msondo unaonya kila kitu, unaweza kupitia hapa.

"Usiendekeze ee moyo utakavyokutuma. Unadanganya jaribu kushinda, usiposhinda, huna budi kumia, utajivisha kitanzi pasipo huruma."

"Kumpenda mke wa rafiki yako kweli ni hatari, viko vitu vya kupenda lakini vingine vina madhara, oooh moyo utakupeleka kaburini. Nakuomba jirekebishe bwana, tabia hiyo siyo nzuri bwana, ni kitendo cha aibu na kashfa ya hali ya juu, tunakusihi sana acha mara moja.

Ulijua huyo ni ndugu yako na rafiki yako swahiba na leo wamasaliti, vipi sasa wanamtamani shemejiyo? Sikio la kufa halisikii dawa."

Hata mwanamuziki Marijani Rajab hakukaa kimya kwenye hili. Miaka ya 1980 alitunga wimbo aliouita 'Mwana Umepotea,' ambao una mashairi haya.

"Mzee Said ee alikuja lalamika ee, kasikia fununu kwamba unavuruga nyumba za watu kaja kutoa onyo anasema kijana ole wako, nasikitika sana ndugu yangu kuwa na mambo hayo, umefanya mambo mengi lakini haya yamezidi kipimo, mchezo na nyumba za watu sawa sawa kucheza na moto. Wacha wacha mara moja, hatari kubwa. Utapoteza maisha baba, na wewe ungali mdogo, hujaiona dunia baba, chonde chonde nakuomba baba."

Kaka anamwambia mdogo wake kuwa mjumbe mzee Said alikwenda nyumbani kwao kulalamika juu ya tabia ya kijana huyo kucheza na nyumba za watu. Maana yake anachukua wake za watu. Marijani akamuasa kuwa tabia hiyo ni sawa na kucheza na moto, matokeo yake atapoteza maisha wakati bado ni kijana mdogo.

Huyu ni kijana wa mwisho aliyedekezwa kiasi kwamba tabia yake ikawa mbaya, akawa anafanya kila kitu kibaya mama wizi na mambo mengine kama ulevi, huku akikingiwa kifua na mama yao.

Matokeo yake sasa akajiingiza kwenye janga la kutamani wake za watu.

"Ewe kipenzi cha mama ee, ewe ndugu yetu kitinda mimba, hebu tizama unavyofanya kwanza. Mbona nakuona unapotea, mama naye mapenzi kazidisha kwako, hata kukukanya anashindwa, anakuacha ufanye unavyotaka mwana.

Sasa imebidi nikueleze, nakwambia kama mimi ni kaka yako, ingawa natambua unanidharau, lakini mimi ndiyo nimeona dunia mwanzo." Hicho ki kipande cha kwanza wimbo huo. Narudia, mke wa mtu ni sumu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

## Wifi Kichefuchefu-9

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

MUME wangu Kassim, wewe mwenyewe unajua kuwa tangu dada yako aachwe na bwana 'ake na tangu arudi hapa amani hakuna. Sema mimi ni mvumilivu tu."

"Kwa hiyo mmegombana naye nini tena? Ndiyo huyo mtoto?"

"Anasema sijui anauliza kuwa haoni mimba, mtoto, wala dalili." Maneno hayo yalimfanya Kassim atikise kichwa na kutoa kicheko ambacho si halisi.

"Hivi dada yako anaweza kuniuliza maswali kama hayo? Yanamhusu nini? Swali hili ilibidi uniulize wewe kama mume wangu."

"Ni kweli, hujakosea kumjibu hivyo! Uko sahihi, mimi ndiyo mumeo niliyekupenda nikakuoa, kwa hiyo usimsikilize mtu yoyote zaidi ya mimi tu mumeo. Mpumbavu dawa yake ukae kimya tu."

"Sawa mume wangu, lakini nakuomba kaa ongea na Havijawa, asinichanganye, nikamchanganya. Masuala ya kunifuatilia mimi siyataki, yeye siyo mama mkwe wangu. Sijabahatika kumkuta mama mkwe wangu, ameshafariki, yeye nani? Kuna siku utakuja humu ndani utakuta nishamvuruga dada yako na mimi nisharudi kwetu. Siyo kwa kukimbia ndoa, ila kuogopa mkono wa sheria!"

"Ina maana unampiga?"

"Yeye mwenyewe keshanitishia maisha eti nitamfahamu kama yeye ndiyo Havijawa au nani. Ana maana gani?"

Maneno ya mkewe na ambayo ameambiwa ameyasema dada yake walimtisha zaidi Kassim kuliko hata matendo yenyewe. Akaona wanapokwenda mkewe Sauda na dada yake Havijawa si kuzuri.

***************************************

"Hodi nyumba hii, shoga Havijawa upo?" Sauti ilisikika kutoka nje.

Havijawa aliifahamu sauti hiyo ni ya nani, akatoka ndani haraka.

"Karibu shoga yangu Fatuma." Akamribisha.

"Nakaa basi, nimekuja kuulizia ratiba zinasemaje?"

"Za vikoba?"

"Hizo hizo kwa sababu wiki hii mimi sikwenda."

"Na kama ulijua, mida yenyewe ndiyo hii ya kwenda, nisubiri kidogo kikavae twende."

Mgeni akakaribishwa ndani na kukaa varandani akimsubiri.

Baada dakika kadhaa, Havijawa alitoka ndani akiwa amevaa mithili ya mwanamke wa Kinigeria na mkoba wake.




**"Mhh! Yamenikuta mimi hayo shoga. Bwana'angu kaniahidi kunitumia pesa saa nane, mama we, ikatumwa saa kumi kasoro dakika tano, hukuwepo malaika wako alikuwepo, pamoja na jitihada zangu zote, maana nilikuwa nimeshafika vikobani, kwenda kutoa dukani mbali, nikawaambia wanipe namba niwaingizie, muda ukawa umeshapita dakika tatu na hata hakukubaki."**

"Twende shoga kabla muda wa haijaisha, maana wale saa 10:00 kamili usipopeleka rejesho basi hawapokei tena, wiki ijayo ukipeleka faini juu." Havijawa alimkumbusha shoga yake Fatuma.

"Mhh! Yamenikuta mimi hayo shoga. Bwana'angu kaniahidi kunitumia pesa saa nane, mama we, ikatumwa saa kumi kasoro dakika tano, hukuwepo malaika wako alikuwepo, pamoja na jitihada zangu zote, maana nilikuwa nimeshafika vikobani, kwenda kutoa dukani mbali, nikawaambia wanipe namba niwaingizie, muda ukawa umeshapita dakika tatu na hata hakukubaki."

"Pole weee!" Havijawa alimwambia Fatuma, halafu kama vile ilikuwa amesahau kitu.

"Saudaaa!" Akaita kwa ukali.

Muda mfupi baadaye Sauda alitoka chumbani kwake kusikiliza alichoitiwa. Lakini ni kama hakufurahiwa na uitaji wa wifi yake. Macho yake yaliongea kila kitu kwa jinsi alivyokuwa akimtazama Havijawa.

Havijana naye alipoyaangalia macho alijua kuwa wifi yake amekasirika. Hakujali.

"Mimi natoka, naenda kwenye vikoba. Vyombo uoshe japo leo ni zamu yangu, halafu hapa varandani upige tena deki, pamechafuka, ukimaliza madirisha nayo yamechakuwa machafu, usafishe, umesikia?" Sauda hakujibu kitu. Akabaki amemtumbulia macho wifi yake.

"Hujibu kitu! Jeuri eee ya kwenu eee! Mijitu mingine bwana, sijui ikoje! Hebu shoga yangu twende zetu, asiniharibie siku tu hapa."

***************************************

"Enhee afadhali nimekuona kaka yangu."

"Hee! dada Fatuma, mbona huonekani nyumbani sana siku hizi?"

"Mambo mengi kaka yangu, maisha yameshakuwa magumu, ile juzi nilikuja sikukukuta."

"Lakini ukimkuta wifi yako na rafiki yako ni kama umenikuta mimi tu."

"Ni kweli nimewakuta wote, lakini nilichokiona pale kaka sikukipenda!" Jibu hilo kidogo lilimshtua Kassim. Alishaanza kuona dalili kuwa huenda dada yake na mkewe waligombana mbele ya mgeni.

Anajua kila kitu kinachofanyika nyumbani kwake kati ya watu hao wawili, lakini hakudhani kuwa hata siku moja wanaweza kuonyesha tofauti zao mbele ya wageni.

Kassim alikuwa amekutana na Fatuma njiani. Dada yule aliyekwenda kumfuata Havijawa kwenda vikobani.

"Kitu gani hukukipenda?"

"Yule dada yako, mbona hana adabu kwa mkeo? Nimefika mimi pale muda mfupi, alivyomwita, alivyokuwa anampa hayo maagizo sijui afanyie, asafishe madirisha kama mtoto mdogo, au binti yake, kweli hiyo?"

"Yaani mimi nimeshachoka dada yangu Fatu, bora na wewe umwambie."

"Siyo nimwambie, wewe mwanaume bwana, ikilemaa hata nakwambia mke huna. Ipo siku atakasirika yule, ataondoka na kukuacha na dada yako mbaki mnatumbuliana macho."

"Mimi nalijua hilo, na nimeshamwambia mke wangu kuwa mvumilivu..."

"Pale hakuna cha uvumilivu, mke atashindwa yule. Nimekaa dakika tano tu kwako lakini nilichokiona kusema kweli hakijanipendeza, yule mke mvumilivu kama mimi nisingekubali."

"Sasa dada yangu unanishauri vipi?"

"Havijawa ni shoga yangu, lakini kwa alichomfanyia yule dada sijakipenda, na nadhani yake ndiyo maisha yao, au imetokea siku hiyo?"

"Huwa naambiwa vitu vingi sana Havijawa wanamfanyia wifi yake, ila huwa nambembeleza tu, yanaisha."

"Hapana, ni lazima uongee na dada yako, au ufanye kitu ambacho kitamaliza hili tatizo, vinginevyo jiandae kumkosa mke."

"Ndiyo maana narudia pale pale, hebu nipe ushauri wako dada."

"Mimi siwezi kukupa ushauri wa kumkandamiza mkeo, au dada yako. Uamuzi unao mwenyewe kaka kusuka au kunyoa."

***************************************

"Samahani dada kama nakufananisha!" Sauda alisikia sauti nyumba yake.

Akawa anajiuliza ni nani anayemfananisha huku sokoni.

Akageuka na kukutana na sura ya dada mmoja ambaye ni kama aliwahi kumuona sehemu fulani lakini hakumbuki.

Yeye hakutaka kumwambia kuwa kama aliwahi kumuona sehemu fulani, akabaki kumtazama tu ili ajitambulishe.

"Wewe ndiyo mke wa Kassim eee?" Sauda alisita kidogo kwa sababu hakujua lengo la dada huyo ni nini, lakini kuna kitu kikamwambia hakuna baya, akubali.

"Ndiyo mimi!"

"Ooh vizuri, mimi ndiyo yule dada aliyekuja wiki ilee pale nyumbani kwenu, nilimfuata wifi yako tukaenda vikobani. Naitwa Fatuma."

Hapo ndipo Sauda alipofunguka macho, akikiri ni kweli kabisa ndiye yeye. Na ndiyo maana akili yake ilimwambia kuwa mtu huyu ameshawahi kumuona mahali.

"Ahaaa kweli, nimeshakutambua."


INAENDELEA JUMAPILI

# NANDI, KIBA KIMAHABA ZAIDI

WANAMUZIKI wanaotamba katika Bongo Fleva, Nandi na Ali Kiba, wameonyesha kwamba wao wana nguvu kubwa katika suala la burudani baada ya wimbo wao mpya kuibuka kinara.

Wimbo huo unaoitwa Dah, ambao una siku mbili tangu kuachiwa rasmi, lakini umeonekana kutamba katika majukwaa ya muziki na kushika namba moja kati ya nyimbo zilizoachiwa mwezi Februari.

Katika mtandao wa You Tube kibao hicho kimefanya vizuri kwa kuwa na watu zaidi ya milioni 1.5 waliogusswa nao na walioutazama ni 500,000.



# MASTER JAY KAWACHAMBUA

MTAYARISHAJI mkongwe wa muziki nchini ambaye pia ni jaji wa shindano la kuibua vipaji la Bongo Star Search, ameibua sintofahamu baada ya kuwaweka katika madaraja mawili wasanii wakubwa Diamond Platnumz na Ali Kiba.

Akizungumza na radio ya East Africa, Master Jay amesema wasanii hao wenye wafuasi wengi nchini kila mmoja ana uwanja wake na hakuna mtu wa kushindana nao.

Amesema tofauti yao kubwa ni Diamond amejizatiti kama mburudishaji bora na Ali Kiba amesimama kuwa mwimbaji mahiri.

Akazidi kuchambua kwamba Kiba amekuwa mwamba katika kutunga na kuimba, huku Diamond ni mzuri katika majukwaa kutokana na ubunifu wa kutumbuiza.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE HAENDI EPL
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 25, hatahamia katika Ligi Kuu England msimu ujao, kwa sababu anatazamiwa kuchagua kati ya klabu ya sasa ya Paris St-Germain na Real Madrid. (***Caughtoffisde***)

### ARTETA: RAMSDALE HAONDOKI
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ananuia kumbakisha kipa wa Timu ya Taifa ya England, Aaron Ramsdale, mwenye umri wa miaka 25, katika klabu hiyo kwa siku zijazo. (***Football Transfers***)

### AMORIM ANUKIA LIVERPOOL
LIVERPOOL wamejua Kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, mwenye umri wa miaka 39, atakuwa tayari kujadili uwezekano wowote wa kuhama msimu ujao. (***Teamtalk***)

### ROONEY KWENDA SAUDIA
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney, ameonyesha nia ya kufuata nyayo za mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya England, Steven Gerrard, kuinoa moja ya klabu za soka za Saudi Arabia. (***Sun***)

### DE GEA ALITAKIWA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest ilimpa mlinda mlango wa zamani wa Manchester United, David De Gea, mwenye umri wa miaka 33, njia ya kurejea kwenye soka kabla ya muda wa mwisho wa kufungwa kwa dirisha la usajili. (***Athletic***)

### WOLVES KITANZINI EPL
GARY O'Neil amesema Wolverhampton Wanderers itakabiliwa na uwezekano wa kukatwa pointi 10 msimu ujao kwa kukiuka sheria za matumizi ya fedha. (***Mail***)

### MAINOO ATAKIWA GHANA
KIUNGO wa kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo, mwenye umri wa miaka 18, analengwa na Chama cha Soka cha Ghana, ambacho kinamtaka abadili uraia wake baada ya kuchezea timu za vijana za England. (***Telegraph***)

### LINGARD AGEUKA LULU
KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 31 ana ofa kutoka kwa takriban klabu 26 kote ulimwenguni. (***Mail***)

### GIL AFURAHISHA SPURS
KIUNGO wa kati wa Tottenham Hotspur na Hispania, Bryan Gil, mwenye umri wa miaka 22, aliamua kutokubali pendekezo lolote la mkopo wakati wa dirisha la usajili la Januari, licha ya klabu mbalimbali ikiwamo Brighton kutaka kumsajili. (***Fabrizio Romano***)

### MOURINHO AWAKATAA WAARABU
KOCHA wa zamani wa AS Roma, Jose Mourinho, amekataa ofa ya kuwa kocha wa klabu ya Al-Shabab inayoshiriki Ligi Kuu Saudi Arabia. (***Standard***)

### CALAFIORI ATAJWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur bado imeonyesha nia ya kutafuta dili la mlinzi wa Bologna na Timu ya Taifa ya Italia, Riccardo Calafiori, mwenye umri wa miaka 21 msimu wa joto. (***Teamtalk***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DRC: TUNALITAKA KOMBE LA AFCON

**ABIDJAN,** Ivory Coast

**Mshambuliaji wa timu hiyo afunguka wachezaji wako tayari...**

MSHAMBULIAJI wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Yoane Wissa, amesema kikosi chao kimedhamiria kubeba bendera ya taifa lao juu baada ya kujikatia tiketi ya kucheza hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

Wissa alifunga penalti muhimu wakati DRC ilipoilaza Guinea mabao 3-1 katika mechi ya hatua ya robo fainali iliyochezwa juzi.

Mshambuliaji huyo anayeichezea Klabu ya Lorient, ambaye alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo, alisema ni heshima kujitokeza kwa ajili ya nchi yake inapohitajika.

"Ninapenda kuchukua majukumu haya, kama wachezaji wenzangu wote - sisi ni wanaume na tunataka kubeba bendera ya nchi yetu hadi kiwango cha juu," alisema Wissa akiwaambia waandishi wa habari.

> **"Niko tayari kucheza popote, safu ya ushambuliaji, kiungo, ulinzi. Wakati nchi yangu inaniita, lazima niwepo. Ninajivunia kuwa Mkongo."**

DR Congo wanawinda taji la tatu la AFCON na la kwanza tangu walipochukua ubingwa huo mwaka 1974.

Wissa alisema kikosi chake hakina upendeleo juu ya nani watakayemfuata kwani wanakaribia fainali.

"Iwe ni Mali au Ivory Coast, hatuna tatizo. Ni mataifa mawili makubwa ya soka na tunapaswa kuwa tayari kwa ajili yao," alisema.

Timu nyingine iliyofuzu hatua ya nusu fainali ni Nigeria ambayo iliwachapa bao 1-0 Angola.

# SIMON: KUSHINDA NDIO MUHIMU KWA NIGERIA




**ABIDJAN,** Ivory Coast

WINGA wa Nigeria, Moses Simon, amesema ushindi wa timu ni muhimu zaidi kuliko sifa za mtu binafsi baada ya kutawazwa kuwa mchezaji bora wa mechi katika ushindi wao wa robo fainali dhidi ya Angola katika mechi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), iliyochezwa juzi usiku.

Simon alitengeneza bao la ushindi la kipindi cha kwanza lililofungwa na Ademola Lookman ambalo lilihitimisha ushindi wa 1-0 na kuwapeleka Super Eagles katika hatua ya nusu fainali.

Mchezaji huyo wa Nantes alipewa tuzo ya mchezaji bora wa mechi, lakini alisisitiza mafanikio ya pamoja ndio yaliyopewa kipaumbele.

"Nina furaha sana, lakini jambo muhimu zaidi ni tulishinda," alisema Simon akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi hiyo.

"Unaweza kuwa mchezaji bora wa mechi na timu yako ikapoteza mchezo."

Simon pia alimuunga mkono mshambuliaji Victor Osimhen ambaye alifunga bao, lakini likakataliwa.

"Mazingira ni mazuri katika timu. Osimhen anafikiria kushinda, sio kufunga tu," alisema.

"Iwapo atapata nafasi ya kufunga ataichukua, lakini anazingatia ushindi wa timu kwanza."

Simon mwenye umri wa miaka 28 alishinda tuzo yake ya pili ya mchezaji bora wa mechi kwenye michuano hii baada ya pia kupata tuzo dhidi ya Guinea-Bissau katika hatua ya makundi.

Asisti yake kwa mfungaji Lookman ilikuwa mchango muhimu kwa Nigeria ilipofuzu hadi nne bora katika harakati zake za kuwania taji la nne la Afrika.

# Xavi hajawahi kuwa na furaha Barca

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández amesema moja ya sababu kuu ya yeye kuamua kuachia ngazi mwishoni mwa msimu huu ni kutofurahia kazi yake kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa.

Xavi mwenye umri wa miaka 44 alitangaza kuondoka klabuni hapo baada ya kufungwa 5-3 wikendi iliyopita na Villarreal, ataondoka Barca mwishoni mwa msimu licha ya kuwa na mkataba hadi mwaka 2025.

"Ninaondoka kwa sababu imekuwa miaka miwili na nusu sasa na ninahisi kama hakuna fidia ya kuwa kocha wa Barca," alisema katika mkutano na wanahabari kabla ya mchezo wa jana LaLiga huko Alavés. "Unapambana na mambo mengi na yanakuchosha, hufurahii siku hadi siku, hata mimi nimeiona kwa makocha walioshinda hapa pia.

"Katika klabu nyingine, kuna fidia. (Kocha wa Osasuna Jagoba) Arrasate aliniambia anafurahia Jumatatu hadi Ijumaa. Sifanyi hivyo; hiyo ndiyo tofauti kubwa. Sifurahii Jumatatu hadi Ijumaa.

"Nchini England, Ujerumani na mataifa mengine nina uhakika wanafurahia taaluma hiyo. Hilo ndilo nililomwambia rais. Nimekuwa mkweli na kuanzia Juni 30 kunahitajika mabadiliko bila shaka."

Kipigo hicho kutoka kwa Villarreal kiliiacha Barca pointi 10 nyuma ya vinara wa LaLiga, Real Madrid.

Hata hivyo, Xavi, ambaye alichukua mikoba ya Ronald Koeman mnamo 2021, aliiongoza Barca kutwaa taji la LaLiga na mafanikio ya Supercopa msimu uliopita, mambo ambayo anahisi yamesahaulika nchini Hispania.

"Nje ya Hispania, kazi tuliyofanya inathaminiwa sana, na watu wa kweli wa mpira wanaofanya kazi kwenye mchezo," aliongeza.

"Kila mtu anatupongeza kwa kazi tuliyofanya. Hata makocha wengine kwenye LaLiga kama wa Real Sociedad Imanol Alguacil, wa Villarreal Marcelino, Arrasate... Lakini hapa Hispania haijathaminiwa."

Barca bado wana nafasi ya kumaliza msimu wakiwa na hali nzuri. Kuna mechi 16 za LaLiga, kuanzia na Alavés, na watamenyana na Napoli katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya

"Tumefanya kazi nzuri na bado tunatumaini kumaliza kwa kiwango kizuri," alisema Xavi.

"Madaraja yatatolewa mwishoni mwa msimu na mzunguko wangu utakamilika Juni 30.

"Kwa tangazo lililotolewa, nadhani mambo yatatuendea vyema. Yeyote anayesema wachezaji watapumzika hajakaa kwenye chumba cha kubadilishia nguo. Unaweza kuelewa ikiwa umecheza soka."

Wakati huo huo, orodha ya majeruhi ya Barca inaendelea kukua, huku Ferran Torres akiungana na João Félix, Raphinha, Gavi, Sergi Roberto, Alejandro Balde, Marcos Alonso na Marc-André ter Stegen wakiwa nje ya uwanja baada ya kuumia katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Osasuna Jumatano.

## Ten Hag : Nilikosa mshambuliaji

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema "sio siri" alitaka kusajili mshambuliaji katika dirisha la Januari na anakiri anaweza kuwa "mbunifu" linapokuja suala la kusuluhisha ukosefu wa wafungaji ndani ya Manchester United.

Ten Hag alisema kanuni za kifedha kwenye Ligi Kuu England, ulifanya klabu hiyo kushindwa kusajili mshambuliaji katika dirisha hilo lililopita.

Kumpoteza Anthony Martial kwa zaidi ya miezi miwili kutokana na majeruhi kumemfanya Ten Hag kubaki na Rasmus Højlund pekee ambaye ndiye mshambuliaji mkuu katika kikosi chake kwa kipindi cha pili cha msimu.

"Nadhani sio siri nilitaka mshambuliaji wa ziada kwa sababu kwa kuumia kwa Martial hatuna msaidizi," Ten Hag alisema.

"Haikuwezekana kwa sababu tunapaswa kuendana na sheria za FFP. Tuna Omari Forson, tuna Amad Diallo, au bila shaka tunaye Marcus Rashford ambaye anaweza kucheza huko. Nafasi zingine zimekaliwa lakini lazima ubunifu kidogo katika namba tisa."

United wana matumaini kwa kuruhusu wachezaji kadhaa, akiwamo Donny van de Beek na Jadon Sancho, kuondoka katika klabu hiyo kwenye dirisha la Januari watakuwa na uhuru zaidi wa kusajili wachezaji bila kukiuka kanuni.

Ten Hag, hata hivyo, anasema hakubaliani kabisa na sheria hizo, ambazo anaamini zilazimisha klabu kuwaondoa "wachezaji wazuri".

"Kuna baadhi ya hasara na FFP," alisema.

"Ili kutengeneza nafasi kwa FFP, lazima uuze wachezaji na lazima uuze wachezaji wazuri na sidhani kama hivyo ndivyo unavyojenga timu."



# DIDA AITABIRIA NAMUNGO ITASHIRIKI MICHUANO CAF

**Na Adam Fungawango**

KIPA wa Namungo FC ya Lindi, Degratius Munishi 'Dida', ameitabiria timu yake itapata nafasi ya kucheza mashindano ya kimataifa katika msimu ujao kutokana na ubora walionao.

Dida, ambaye amezichezea timu mbalimbali nchini zikiwamo vigogo Simba na Yanga kwa misimu tofauti, alisema kwa namna ambavyo wamejidhatiti anaamini msimu ujao wana nafasi ya kupata tiketi mojawapo ya kuchuana katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho.

"Kwanza kabisa nikwambie hayo ndiyo malengo tuliyojiwekea kuanzia viongozi mpaka wachezaji. Ni kurejea kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, na kitakachosababisha hivyo ni kushika nafasi nne za juu wakati msimu wa ligi utakapomalizika.

Kuwa na malengo kitu kimoja na kutekeleza ni kitu kingine, lakini kwa jinsi nilivyoona maandalizi yetu, naamini kabisa tutacheza michuano ya CAF," alisema Dida.

Aliongeza moja ya vitu ambavyo vinamfanya awe na matumaini makubwa ni uwepo wa Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, ambaye amejiunga hivi karibuni akitokea Coastal Union.

"Tuko na kocha mpya (Zahera), ni kocha mzoefu, amefundisha timu kadhaa ikiwamo Yanga, analielewa soka la Tanzania, siyo mgeni hapa nchini na anajua wachezaji wa Kitanzania jinsi walivyo, hapa tumeshacheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Mashujaa FC na Malimao FC, ambazo zote tumeonyesha mwelekeo mzuri nadhani tukirudi katika ligi tutaonyesha dhamira yetu," alisema golikipa huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Kwa sasa Namungo ipo Dar es Salaam kwa ajili ya kambi na mechi mbalimbali za kirafiki ili kujiimarisha, itashuka dimbani Februari 11, mwaka huu kuwakabili Tabora United kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Namungo yenye pointi 17 iko kwenye nafasi ya nane, wakati mara ya mwisho kucheza mashindano ya kimataifa ilikuwa ni mwaka 2021, na ilitolewa hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

## Dodoma Jiji FC yaitishia Yanga

**Na Oliver Albert**

WAKATI Dodoma Jiji ikiendelea kujiimarisha katika kambi yake mkoani Morogoro, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Francis Baraza, amesema yuko tayari kuhakikisha anafuta rekodi 'mbaya' dhidi ya Yanga.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Yanga wataikaribisha Dodoma Jiji kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Baraza alisema anajua timu yake haijawahi kupata ushindi dhidi ya Yanga tangu ipande daraja mwaka 2020 lakini sasa ni wakati wa kupambana kufuta rekodi hiyo.

Dodoma Jiji tangu ipande Daraja Julai 2020 kucheza Ligi Kuu imekutana na Yanga kwenye ligi mara sita, imefungwa mara tano na sare moja.

"Tunaendelea kujiandaa tukiamini itakuwa mechi ngumu kwa sababu tunakutana na mabingwa watetezi ambao pia wana kikosi kizuri sana.

Nafurahi jinsi wachezaji wangu walivyo na morali kubwa mazoezini na wanaonekana wana ari kuelekea mchezo huo ambao ni lazima tupambane ili kupata matokeo mazuri," alisema Baraza.

Dodoma Jiji iko katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 18 baada ya kucheza michezo 13, imeshinda mitano, imetoka sare michezo mitatu na kupoteza mitano.






Wachezaji chipukizi wakifanya mazoezi ili kuboresha viwango vyao kwenye viwanja vya JKM Park jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## New City FC walia kupoteza umakini

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufungwa bao 1-0 na JKU katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi jioni, New City FC imesema matokeo hayo yametokana na wachezaji wake kupoteza umakini.

Bao pekee la ushindi kwa Maafande wa JKU SC lilipachikwa na Shabaan Pandu dakika ya 45.

Kocha wa New City, Razak Rajab, alisema timu yake ilifanikiwa kutawala mchezo katika dakika zote za kipindi cha kwanza lakini wachezaji wake hawakuwa makini uwanjani.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi ambazo zingeweza kuzaa matunda iwapo wachezaji wangekuwa na utulivu na mbinu ya kiujanja, lakini hilo halikufanikiwa.

Kocha huyo aliongeza mchezo huo umemalizika na sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata dhidi ya Hard Rock utakaochezwa Februari 12, mwaka huu huko Pemba.

Naye Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali Haji, alisema licha ya kupata alama tatu lakini wapinzani wao walicheza kandanda safi na kuonyesha upinzani mkali.

# 'Wanasiasa msitumie michezo vibaya'

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

KANISA Katoliki Jimbo la Singida limewatahadharisha wanasiasa nchini kutotumia sekta ya michezo kama sehemu ya kutafutia kura na badala yake wajenge utamaduni wa kuwaandalia vijana mazingira mazuri ya kupata ajira katika siku za baadaye kupitia michezo mbalimbali, imeelezwa.

Mhashamu Baba Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Singida, Edward Mapunda, ametoa tahadhari hiyo na kutaja hiyo ni moja ya sababu zinazochangia timu za taifa kutofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Kiongozi huyo aliweka bayana si kweli wanasiasa wanapoanzisha mashindano ya soka wanalenga kuwaandaa vijana katika ajira lakini badala yake wamekuwa wakijitafutia ajira zao binafsi.

Alisema ili kuondokana na matokeo mabaya kwa timu za taifa, wakati umefika kwa wizara yenye dhamana kutazamwa upya kwa kutengewa bajeti kubwa itakayoweza kusimamia sekta hiyo kwa ubora unaohitajika.

Aliongeza hakuna timu itakayopata ushindi wowote wa ghafla na hakuna sababu zozote za kukata tamaa huku akisema kufanya vibaya kwa wawakilishi wa Tanzania kimataifa kunatokana na mamlaka zinazosimamia sekta ya michezo kutowekeza mapema.


Aliwataka pia wadau mbalimbali wa sekta ya michezo wakiwamo viongozi wa madhehebu ya dini zote waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuanzisha vituo vya michezo.

Michezo
Jumapili Februari 4, 2024
Nipashe

UKU. 21



## DRC: Tunalitaka Kombe la AFCON




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza (kushoto) akiwania mpira dhidi ya nyota wa Mashujaa, Baraka Mtuwi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma jana. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Kagera wairudisha darasani Yanga SC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kugawana pointi na wenyeji, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ameanza kutafuta dawa ya kukabiliana na wapinzani wenye tabia ya kupoteza muda katika mashindano mbalimbali ikiwamo michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Gamondi, alisema hakutarajia timu yake kupata matokeo hayo na akakiri kitendo cha wachezaji wa Kagera Sugar kujiangusha dakika za mwisho kiliharibu mchezo huo.

Gamondi aliasema kipindi cha kwanza kilikuwa na presha kubwa lakini ngwe ya pili walicheza vizuri na walitengeneza nafasi kadhaa za kufunga ingawa wachezaji wake walishindwa kuzitumia vyema.

Kocha huyo alisema mechi hiyo iliharibiwa na wapinzani wao ambao walikuwa wanajiangusha mara kwa mara ili kupoteza muda lakini tayari ameanza kufanyia kazi mapema kwa kutafuta mabao dakika za mapema.



"Siwezi kumlaumu mwamuzi alikuwa sahihi lakini kitendo cha kupoteza mpira kilishusha morali yetu, kinachotakiwa tunapaswa kucheza kama mabingwa watetezi na kushinda michezo iliyo mbele yetu," alisema Gamondi.

Aliongeza kwa kuongeza mbinu, itawasaidia kurekea katika kasi yao ya ushindi na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Fred Minziro, alisema ulikuwa mchezo ngumu kucheza na bingwa mtetezi ingawa waliingia uwanjani wakiwa na malengo ya kupata pointi tatu.

"Wachezaji wangu wamepambana sana, nawapongeza na sasa tunaangalia mechi ijayo ambapo tutahakikisha tunafanikiwa kuvuna alama tatu, tunataka kushinda kila mechi zilizopo mbele yetu," alisema Minziro.

Msemaji wa Kagera Sugar, Hamisi Mzanzala, alisema matokeo waliyopata kwao ni sawa na ushindi na huo ni mwanzo mpya wa ujio wa Minziro katika kikosi chao.

Mzanzala alisema Minziro amebadilisha 'kila kitu' katika timu yao na sasa wanaamini watarejea kwenye ushindani.

# Simba yaizima Mashujaa Bara

## ●●● Huku Ntibazonkiza akiendelea kung'ara baada ya kufunga...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la penalti lililofungwa na kiungo mshambuliaji raia wa Burundi, Saido Ntibazonkiza liliifanya Simba kuondoka na pointi tatu muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mashujaa FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma jana.

Mrundi huyo alifunga penalti hiyo dakika ya 15, baada ya winga machachari wa Wekundu wa Msimbazi, Kibu Denis kubwagwa ndani ya eneo la hatari na Zuberi Dabi wa Mashujaa katika harakati za kumkaba.

Akiwa kwenye wingi ya kulia, Kibu alimlamba chenga, Mpoki Mwakinyuke na kuingia ndani ili kuleta madhara, lakini beki huyo akamfanyia faulo iliyosababisha adhabu hiyo.

Linakuwa ni bao la tano kwa Saido, manne akifunga kwa penalti huku nyingine akipachika katika mechi dhidi ya KMC, Kagera Sugar na Prisons.

Pia linakuwa ni bao la tano kwa Simba kufunga kwa penalti ikiwa ndiyo timu inayoongoza katika Ligi Kuu kwa kupata penalti nyingi mpaka sasa na zote zimekwamisha wavuni.

Ushindi huo unawafanya Wekundu wa Msimbazi kufikisha pointi 26, lakini ikiendelea kuwa katika nafasi ile ile ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa imecheza mechi 11.

Mechi hiyo ilianza kwa timu zote kucheza soka linalofanana, zikipiga mipira mirefu ambayo kwa kiasi kikubwa haikuwa na manufaa yoyote.

Simba ingeweza kuandika bao mapema tu dakika ya tisa, baada ya straika wao mpya, Freddy Michael, alipopata mpira akiwa ndani ya eneo la hatari akitazamana na kipa wa Mashujaa, Erick Johora, alipiga shuti kubwa lililopaa juu.

Staika huyo alikutana na mpira huo uliotokana na Dabi kutaka kumpiga chenga, Israel Mwenda lakini ulimbabatiza na kumfikia akiwa ndani ya sita, lakini akakosa.

Baada ya bao la dakika ya 15, nusura Simba ipate bao la pili dakika ya 21, wakati Freddy alipowahadhaa mabeki wa Mashujaa na kuachia shuti lililopanguliwa na Johora, huku mpira uliporudi ulimkuta Kibu, alkini shuti lake liliwababatiza mabeki wa timu hiyo na kurejea uwanjani.

Ntibazonkiza kama angetulia angeweza kufunga bao dakika ya 31, lakini alikuwa na papara akiwa ndani kidogo ya eneo la hatari, alipiga shuti dhaifu lililoishia mikononi mwa Johora.

Vijana wa Mohamed Abdallah 'Bares' waliingia kivingine kipindi cha pili kwa kucheza kwa kasi, na dakika tatu tu baada ya mapumziko, walifanikiwa kupiga shuti la kwanza langoni kwa Simba kupitia kwa Omari Omari, lakini mpira ukatoka nje.

Omari kwa mara nyingine tena alifanya shambulizi katika lango la Simba baada ya mpira uliokosewa na Mzamiru Yassin, lakini shuti lilipaa juu ya lango.

Nafasi nzuri zaidi kwa Mashujaa FC kusawazisha bao likuwa dakika ya 65, wakati mpira wa faulo uliopigwa na Abrulrahman kuunganishwa kwa kichwa na Dabi, lakini mpira ukaenda kugonga mwamba wa juu la lango la Simba na kutoka nje.

Dakika 45 za pili angalau Manula alionekana yupo kazini, ambapo dakika ya 80 aliruka juu kuokoa mpira wa kichwa uliopigwa na Emmanuel Mtumbuka uliokuwa ukielekea wavuni.

Maafande hao wamesalia na pointi zao tisa na kubakia kwenye nafasi ile ila ya 15 ikishuka dimbani katika michezo 13.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >